# Nipashe

Jumatano Februari 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580494

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Sababu** kutofikiwa malengo makusanyo Zanzibar yaanikwa

UKURASA 3



**Operesheni** ya polisi yanasa silaha na watuhumiwa vitendo vya ujangili

UKURASA 4




**Costa akaribia kutua Palmeiras**

UKURASA 21

# Vigogo 20 Maji watumbuliwa

UKURASA 2





Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akishiriki sala ya kuuombea mwili wa marehemu Mohammed Seif Khatib, iliyoongozwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi (mbele), katika Masjid Noor Muhammad S.A.W, kabla ya mazishi yaliyofanyika kijijini kwao Umbuji, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja jana. Kushoto ni Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na (wa pili kushoto) ni Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla. **Habari Uk.4. PICHA: IKULU**

## EU yaipa Tanzania mabilioni

UKURASA 2

## Wadaiwa sugu wa matrekta waingia matatani TAKUKURU

UK. 3

Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

**MICHEZO** **MTIBWA YAMHOFIA KATWILA IKIIVAA IHEFU** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Ulaya yaimwagia Tanzania bilioni 308/-

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI ya Tanzania imesaini mikataba sita na Umoja wa Ulaya (EU) yenye thamani ya Sh. bilioni 307.9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na umoja huo.

Miongoni mwa miradi hiyo ni uboreshaji wa nishati, kusaidia mnyororo wa thamani kwenye ufugaji nyuki, mazingira ya biashara na ubunifu na mradi wa ushirikiano wa kitaalamu.

Mikataba hiyo ilisainiwa jana ambapo Tanzania iliwakilishwa na Katibu Mkuu wa Wizara Fedha na Mipango, Dotto James, huku EU ikiwakilishwa na Balozi wake nchini, Manfredo Fanti.

Akizungumza baada ya kusaini mikataba hiyo, Katibu Mkuu huyo alisema fedha hizo ni za miradi maendeleo, ambazo zimetolewa kupitia Mpango wa Ushirikiano wa 11 chini ya Mfuko wa Maendeleo wa Ulaya (EDF).

"Naomba Watanzania wenzangu tuelewe kuwa mikataba hii tuliosaini leo, fedha hizo Euro 111.5 sawa na Sh. bilioni 307.9 ni msaada wa miradi hii inayofadhiliwa na umoja huu na sio mkopo," alisema.

Alifafanua katika mradi wa kuboresha sekta ya nishati umepokea Sh. bilioni 96.7 na mradi wa matumizi endelevu ya nishati ya kupikia umepata Sh. bilioni 82.2.

Aliitaja miradi mingine ni wa kusaidia mnyororo wa thamani katika ufugaji nyuki ambao umepata Sh. bilioni 27.6 na wa kuboresha huduma ya afya ya mimea ili kuongeza usalama wa chakula Sh. bilioni 27.6.

"Miradi mingine ni wa kusaidia kuboresha mazingira ya biashara, ukuaji na ubunifu Sh. bilioni 63.5 na wa ushirikiano wa kitaalamu Sh. bilioni 9.7," alisema.

Aidha, alisema tangu kutiwa saini mkataba wa kwanza wa ushirikiano kati ya EU na nchi za Afrika, Caribbean na Pasific (ACP) mwaka 1975, Tanzania imepokea kutoka umoja huo takribani Sh. trilioni 6.6 kama misaada.

Kadhalika, alisema Tanzania imepokea Sh. bilioni 748 .2 kama mikopo yenye masharti nafuu kutoka benki ya uwekezaji ya Ulaya (EIB) na fedha hizo zilizotolewa zimekuwa chachu ya maendeleo ya maeneo mbalimbali nchini na kusaidia ukuaji wa uchumi.

Alishukuru umoja huo kwa misaada yake nchini kwa kuwa imetolewa wakati mwafaka ambapo serikali inaweka mazingira wezeshi ya kukuza viwanda kwa ajili ya ukuaji wa uchumi.

Alibainisha kuwa wizara hiyo itaendelea kutoa mwongozo unaohitajika ili kuhakikisha kuwa fedha zinazotolewa zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Balozi Fanti alisema lengo la misaada hiyo ni kuboresha maisha ya wananchi na kusaidia kukuza uchumi wa nchi.

Alisema pia fedha hizo zitasaidia kuzalisha bidhaa bora ambazo zitakuwa na uhakika wa soko la biashara kwenye umoja huo wa nchi za Ulaya.

Alitaja sababu ya kutoa misaada hiyo kuwa ni kutokana na kuridhishwa na mapato na matumizi ya Tanzania yaliyoiwezesha kuingia kwenye uchumi wa kati.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James (kushoto), akibadilishana nyaraka na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) hapa nchini, Manfredo Fanti, jijini Dodoma jana, baada ya kutiliana saini mikataba sita yenye thamani ya Euro milioni 111.5 sawa na Sh. biilioni 307.9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na umoja huo nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**


**NAMPULA AUCTION MART AND COMPANY LTD**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **NBC BANK TANZANIA** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana Za wadaiwa wao ambao wameshindwa kulipa deni wanalodaiwa na banki hiyo.

Mnada utafanyika mahari nyumba/dhamanazilipo

| Jina la mdaiwa | Jina la zamana | Dhamana | Maelezoyadhamana | Tareheyamnada |
|---|---|---|---|---|
| LOLITA PAFYUMERIE | LOLITA LUDOVICK MACHA/LOLITA PAFYUMERIE | NYUMBA | Ct no 120849 ,L.O NO 352472,PLOT NO237 BLOCK 11 KIBADA MANISPAA YA TEMEKE I.N.O LOLITA LUDOVICK MACHA | 10/3/2021 |
| ZUBERI .S .ZUBERI | ZUBERI .S NYARI | NYUMBA | CT NO 10014 LR MOSHI L.O.NO. 136103 PLOT NO 127,BLOCK "N'SECTION IV MAJENGO MANISPAA YA MOSHI,I.N.O | 6/3/2021 |
| WASWARD .W. MAPANDE | YUSUPH WILISONI MMBAKWENI | NYUMBA | CT NO 31283 LR.MOSHI L.ONO 192433 PLOT NO 349 BLOCK "B" HIMO URBAN AREA MOSHI DISTRICT I,N,O YUSUPH WILSON MMBAKWENI | 6/3/2021 |
| LASWAY TRUCK | EDWARD EPIMAK | NYUMBA | PLOT NO 215, BLOCK "G" TEGETA MANISPAA YA KINONDONI DAR ES SALAAM | 10/3/2021 |
| LASWAY TRUCK | EDWARD EPIMAK | NYUMBA | PLOT NO 35-36; BLOCK "KKK"KARANGA MOSHI. | 6/3/2021 |

**Masharitiyamnada**

(a ) Mnunuzi atalazimika kulipa 25%ya beiliyofikiwa katika mnada papo hapo asilimia iliyobakia .75%italipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo.

(b) Endapo mnunuzi atashidwa kulipa asilimia 25% siku ya mnada basi mshindiwa pili anahaki ya kuweka hela siku hiyohiyo .

©mnunuzi akishidwa kutimiza sharti la 75% malipo ya awali hayatarejeshwa no mnada utarudiwa

(d) Gharama za kubadilisha umiliki,kumtoa mtu kwenye nyumba na gharama nyingine zozote zitakazojitokeza itakuwa juu yamnunuzi. .gharama zozote zitakazojitokeza nje ya utaratibu wa kibenki hatutahusika nazo.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA DALALI WA BENKI**
**MOBILE: 0782757829, /071944171**


# Vigogo 20 watumbuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza kutenguliwa uteuzi wa viongozi 22 wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kutokana na kuonyesha udhaifu wa kiutendaji na kusababisha utekelezaji wa miradi ya maji kusuasua.

Viongozi hao ni mameneja 20 wa RUWASA ngazi ya wilaya, Meneja wa Wakala huo Mkoa wa Geita na Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi wa RUWASA, Deusdedith Magoma.

Akitoa taarifa ya uamuzi huo jana jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Anthony Sanga, alisema pamoja na mafanikio ya kuongezeka upatikanaji wa maji vijijini kutoka asilimia 64.9 hadi 72.3, imebainika kuwapo tatizo la kiutendaji linalochangiwa kwa kiasi kikubwa na baadhi ya viongozi.

"Udhaifu umejionesha zaidi wakati huu ambapo kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini haiendani na mtiririko wa fedha na hasa zinazotolewa na washirika wa maendeleo," alisema.

Aliwataja viongozi hao kuwa ni Meneja wa RUWASA Mkoa wa Geita ambapo kasi ya utekelezaji wa miradi hairidhishi licha ya ufuatiliaji wa mara kwa mara unaofanywa na uongozi wa juu wa wizara na wakala huo. Vilevile, alibainisha kuwa wa ngazi ya wilaya, Waziri Aweso ameagiza uteuzi utenguliwe kwa viongozi 20 kutokana na miradi kusuasua kwenye Wilaya za Buhigwe, Uvinza, Mbulu, Musoma, Mbarali, Rungwe, Tandahimba, Nkasi, Kishapu, Bariadi, Songwe, Uyui, Misungwi, Magu, Bukoba, Babati, Igunga, Bunda, Ikungi na Newala.

"Waziri Aweso pia ameagiza Bodi ya Wakurugenzi wa RUWASA kuchukua hatua mara moja ya kuwatengua viongozi hao na kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuteua watumishi wa RUWASA walioonyesha bidii na umahiri mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yao," alisema.

Aliagiza ujazaji wa nafasi hizo ufanyike ndani ya wiki moja ili kuhakikisha shughuli za wakala huo hazikwami. Katika hatua nyingine, katibu mkuu huyo alisema Waziri Aweso amemteua Ndele Mwansanga kuwa Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi za Wakala huo. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mbeya.

"Waziri Aweso amemhamisha Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa Mjini, Gilbert Kayange kwenda Mamlaka ya Mbeya Jiji na amemteua David Pallangyo kuwa Mkurugenzi wa Mamlaka Iringa," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Clement Kivagalo, aliahidi kutekeleza kwa haraka agizo hilo la waziri ili kuimarisha Sekta ya Maji.

Alisema RUWASA imetia saini makubaliano kati yake na Idara ya Rasilimali Maji ya wizara hiyo, ili kuhakikisha tatizo la kutokuwa na vyanzo vya maji endelevu linapatiwa ufumbuzi mkubwa.

## HABARI KITAIFA

# Wadaiwa sugu wa matrekta waingia matatani TAKUKURU

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), mkoani Dodoma, imeanza kufuatilia madeni sugu mbalimbali yenye thamani ya Sh. bilioni 1.6, ikiwamo ya watu waliokopeshwa matrekta na Mfuko wa Pembejeo wa Taifa.

Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh. milioni 525 ni cha mfuko huo na Sh. bilioni 1.075 zinafuatiliwa kwenye vyama vitatu vya Akiba na Mikopo (SACCOS) vya jijini Dodoma ambavyo vilikopa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mkuu wa taasisi hiyo Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema tayari TAKUKURU inafuatilia fedha hizo na kuwataka wahusika kurejesha fedha

hizo kwa kuwa zina muda mrefu zipo kwao na kukwamisha utendaji wa mfuko huo.

"Unapochukua matrekta halafu hurejeshi fedha, ile fedha haiwezi kuzunguka na wananchi wengine wanufaike na mikopo ya pembejeo inayotolewa, kwa sababu nia ya kuanzisha mfuko huo haiwezi kutimia na fedha ya serikali inapotea bure," alisema.

Katika hatua nyingine, taasisi hiyo imewafikisha Mahakama ya Wilaya ya Mpwapwa, wahasibu wawili wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa tuhuma mbalimbali na kuwafungulia mashtaka matano ya uhujumu uchumi.

Kibwengo alisema Mhasibu Nicholaus Denis amefunguliwa mashtaka manne ikiwamo ya kughushi nyaraka kinyume na sheria na kanuni za adhabu, matumizi ya nyaraka kumdanganya mwajiri, ubadhirifu na shtaka la nne ni uchepuzi ambayo yote Sheria ya Kupambana na Rushwa Namba 11, 2007.

Mhasibu mwingine ni Michael Abanzi ameshtakiwa kwa kosa la kumsaidia mwenzake kutenda makosa hayo ni kinyume na sheria ya kupambana na rushwa.

Alisema uchunguzi wao unaonyesha washtakiwa walitenda makosa hayo Machi na Aprili 2018, ambapo walitengeneza nyaraka zilizoonyesha zilitumika kununua stationary kwa matumizi ya ofisi jambo ambalo si kweli.

# Sababu kutofikiwa mapato Zanzibar

**Na Mwinyi Sadallah, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Jamali Kassim Ali, amesema serikali imeshindwa kufikia lengo la kukusanya Sh. bilioni 779.4 baada ya kukusanya Sh. bilioni 464.6 (asilimia 59.6) kutokana na athari za maradhi ya corona katika nusu ya kwanza ya mwaka huu wa bajeti. Waziri Jamali alisema hayo jana alipokuwa akiwasilisha hotuba ya mwelekeo wa hali ya uchumi na mpango wa maendeleo katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi.

Alisema katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, serikali ilikadiria kukusanya Sh. trilioni 1.5 yakiwamo mapato ya ndani Sh. trilioni 1.05, mikopo ya ndani Sh. bilioni 3.8 na Sh. bilioni 419, zikiwa ruzuku na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo. "Mheshimiwa Spika kutokana na athari ya maradhi ya corona kwa kipindi cha miezi sita Julai mpaka Desemba, serikali imekusanya Sh. bilioni 464.6 sawa na asilimia 59.6 ya malengo," alisema. Waziri Jamali alisema serikali katika kukabiliana na janga la corona, imechukua hatua saba za kuimarisha uchumi ikiwamo kupunguza masharti na kuanza kuruhusu baadhi ya shughuli za kiuchumi kufanyika kama kawaida Zanzibar. Alizitaja hatua nyingine kuwa ni kuruhusu kupokea watalii kutoka nje ya nchi, safari za ndege kuingia na kutoka nje ya nchi, kuruhusu shughuli za biashara za ndani kuwa wazi kwa nyakati za kawaida, kuendelea kutoa tahadhari za ugonjwa wa corona pamoja na wanafunzi kuendelea na masomo.

Waziri huyo alisema usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi umepungua katika kipindi cha miezi sita kutoka Sh. bilioni 33.8 mwaka 2019 hadi kufikia Sh. bilioni 18.2. Alisema uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umefikia thamani ya Sh. bilioni 4587 kulinganishwa na Sh. bilioni 417.7 mwaka 2019.

Waziri Jamali alisema bidhaa zilizoingizwa Zanzibar, asilimia 51.9 ni bidhaa za biashara, bidhaa za chakula asilimia 18.8 wakati bidhaa za kati zikiwa asilimia 29.3 katika kipindi cha miezi sita ya mwaka wa fedha.

Aidha, alisema ununuzi wa zao la karafuu kutoka kwa wakulima Zanzibar umepungua na kufikia tani 206.5 zenye thamani ya Sh. bilioni 2.8 kutoka tani 1,638.5 zenye thamani ya Sh. bilioni 22.9 mwaka 2019. Kuhusu maendeleo ya Sekta ya Utalii, Waziri Jamali alisema idadi ya watalii walioingia nchini, imepungua na kufikia 102,746 (asilimia 69.4) kutoka watalii 335,374 mwaka 2019 kutokana na athari za corona.

Alisema kwamba, baada ya mlipuko wa virusi vya corona, baadhi ya mataifa yaliweka vizuizi vya safari nje ya nchi kwa raia wake pamoja na kuzuiliwa safari za ndege kabla ya kurejea hali ya kawaida.

Kuhusu wajasiriamali, Waziri Jamali alisema serikali inakusudia kuweka ushuru wa kibali cha mwaka kwa wafanyabiashara wadogo kwa gharama ya Sh. 30,000 badala ya kutozwa ushuru wa Sh. 2,000 kila siku na halmashauri.

Waziri Jamali aliliomba Baraza la Wawakilishi Zanzibar liidhinishe mapendekezo ya makadirio ya bajeti ya Sh. trilioni 1.5 na kutayarisha mwelekeo uchumi, mpango wa maendeleo na bajeti mwaka wa fedha 2021/22.


## EAGLE RECOVERIES LIMITED
## NOTISI/MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA Microfinance Bank Ltd** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA Microfinance Bank Ltd,** kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana za mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya mataganzo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| S/N | JINA | AINA YA DHAMANA | MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | Peter Hedison Temba/Antony Pete R Temba. | Nyumba Nzuri Iliyopo Machinjioni Mianzini. | Saa 3:00 Asubuhi Na Kuendelea |
| 2 | Kassim S. Lipolwile | Kiwanja Kizuri Kilichopo Mlamleni Temeke. | Saa 3:00 Asubuhi Na Kuendelea |
| 3 | Ibrahim Ally Muhogomchungu | Nyumba Nzuri Iliyopo Chanika Tungini Ilala Dar Es Salaam. | Saa 3:00 Asubuhi Na Kuendelea |
| 4 | Ismail Sifuni Elikunda | Nyumba Nzuri Zilizopo Kilungule Na Makangarawe Temeke Dar Es Salaam. | Saa 3:00 Asubuhi Na Kuendelea |
| 5 | Mwita Mahema Chacha | Nyumba Nzuri Iliyopo Magengeni Chamanzi Temeke Dar es salaam | Saa 3:00 Asubuhi Na Kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mnada utafanyika sehemu ilipo dhamana
3. Mnunuzi atakayefika bei ya juu atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya mnada
4. Endapo mteja atashindwa kumaliza 75% ndani ya siku 14 kiasi kilichotolewa awali 25% hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
5. Baada ya kukamilisha malipo yote ni jukumu la mnunuzi kumuhamisha mkazi/wakazi waliopo ndani ya dhamana husika.
6. Gharama za kubadilisha hati miliki (ransfer of ownsership) pamoja na gharama nyingine ni juu ya mnunuzi.

**Wote mnakaribishwa**

**Kwa mawasiliano zaidi piga namba**
**0753 351 588/ 0755 985 844 / 0743448888**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**EAGLE RECOVERIES LIMITED,**
**S.L.P 34462,**
**DAR ES SALAAM,**
**SIMU NA.0753 351 588/ 0755 985 844 /0743448888**
**EMAIL: eaglerecoveries2017@gmail.com**

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.

Kampuni ya MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LTD na MAK RECOVERIESLTD, Kwa idhini tuliyopewa FINCA MICROFINANCE BANK LTD tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na Finca microfinance bank ltd, Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| S/N | KAMPUNI INAYOHUSIKA | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Amani Abduel Msuya | Nyumba | Boko chama – Dar es Salaam |
| 02 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Anna B mosha/ Victoria Didas kundi | Nyumba – haijaisha | Bunju B – Dar es Salaam |
| 03 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Neema C. Mbalafu | Nyumba | Kimara baruti - Dar es Salaam |
| 04 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Emmy Abas Chengula | Mali zako (Dhamana) | Dar es Salaam (Dhamana) |
| 05 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Domonick Erick Shayo | Kiwanja | Tegeta 'A' Goba Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam |
| 06 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Joseph Bina Kisiwani | Kiwanja | Gorani kimara Ubungo- Dar es Salaam |
| 07 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Dismas Reginalidi Rupia | Nyumba | Kilimahewa, wazohili kinondoni – Dar es Salaam |
| 08 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Shani N. Ngwada | Mali zako(Dhamana) | Mali zako(Dhamana) |
| 09 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Jacqueline P. Mossile | Kiwanja | Nyakaasangwe Wazohili- Dar es Salaam |
| 10 | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | Moshi Jumanne Juma | Gari yenye number T 449 AAU Mistubish Canter | Tabata Senene Mkabala na Kituo sheli ya Mafuta Lake Oil |
| 11 | MAK RECOVERIES LIMITED | Stephen C. Semkiwa | Gari Nissan Civilian No.T 105 Bfp | Tanga |
| 12 | MAK RECOVERIES LIMITED | Bimkubwa Omar Said | Kiwanja(Dhamana) | Kange kasera Tanga City |
| 13 | MAK RECOVERIES LIMITED | Ramadhani Issa Chambuli | Kiwanja | Pongwe- Tanga City |
| 14 | MAK RECOVERIES LIMITED | Juma Bakari Hemba | Kiwanja | Tangasisi – Tanga City |
| 15 | MAK RECOVERIES LIMITED | Hanafi B. Masuli | Nyumba na Kiwanja | Mabokweni – Tanga City |
| 16 | MAK RECOVERIES LIMITED | Mary C. Shoo | Nyumba na Kiwanja | Sanawari Pongwe – Tanga city |
| 17 | MAK RECOVERIES LIMITED | Shuufwaa S. Huwel | Kiwanja | Mgobe Korogwe |
| 18 | MAK RECOVERIES LIMITED | Silas S. Ngunda | Kiwanja, Plot 19 (Dhamana) | Tanga City |
| 19 | MAK RECOVERIES LIMITED | Seti Ohilipo Bondo | Block C na Plot 24/26 Block | Neema Tanga City |
| 20 | MAK RECOVERIES LIMITED | Juma Bakari Mswaki | Nyumba Plot No15 Block No.212 | Ngamiani Tanga City |
| 21 | MAK RECOVERIES LIMITED | Omary H. Mwambashi | Dhamana | Tanga City |
| 22 | MAK RECOVERIES LIMITED | Abel Kashanga Yohana | Kiwanja na Nyumba Plot 232, Block P | Kichangani Tanga City |
| 23 | MAK RECOVERIES LIMITED | Salimu Athumani Rashid | Kiwanja na nyumba | Mabawa Tanga City na Kange uzunguni Tanga City |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne(14) kuanzia tarehe ya
mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki(Transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**Kwa mawasiliano zaidifikaOfisiza:**

**MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED,**
**S.L.P62070 DAR ES SALAAM**
**Simu No; 0755 506 970 / 0716 7643 571**

**AU**
**MAK RECOVERIES LIMITED,**
**S.L.P 2052 DAR ES SALAAM,**
**Simu No; 0715 375 474 / 0783 224 965**

# Vigogo wahudhuria maziko ya Seif Khatib

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana aliwaongoza wananchi katika maziko ya Dk. Mohamed Seif Khatib yaliyofanyika kijijini kwake Umbuji, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.

Viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa,dini na serikali pamoja na wananchi walihudhuria katika mazishi hayo ambapo mapema Dk. Mwinyi aliungana nao katika sala ya kumuombea marehemu iliyosaliwa huko Masjidi Noor Muhammad (S.A.W), Mombasa kwa Mchina, mjini Zanzibar.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria katika mazishi hayo ni Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, Rais wa Zanzibar mstaafu, Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mstaafu Balozi Seif Ali Idd na viongozi wengine wa serikali na vyama vingine vya siasa.

Akisoma wasifu wa marehemu Dk. Mohamed Seif Khatib huko Umbuji, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Khamis Abdalla Said, alisema Khatib ambaye kifo chake kilichotokea juzi katika Hospitali ya Al-rahma jijini Zanzibar baada ya kuugua kwa muda mfupi, ameoa na kubahatika kuwa na watoto sita.

Alisema kuwa katika elimu, marehemu alijiendeleza sana kielimu na kutunukiwa shahada mbalimbali ikiwamo Shahada ya Ualimu ya Chuo cha Ualimu Nkrumah Zanzibar, Shahada ya Kwanza ya Elimu, Chuo Kikuu cha Dar-es Salaam, Shahada ya Uzamili katika Sanaa, London University SOAS na Shahada ya Uzamivu ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

# Tanzania, Burundi zajadili kutumia rasilimali madini

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

SERIKALI ya Tanzania na Burundi zimeanza majadiliano ya namna ya kutumia rasilimali ya madini yanayopatikana katika nchi zote mbili, katika ukuaji wa uchumi wa nchi hizo.

Majadiliano hayo yalifanyika jana mkoani Kigoma yakijumuisha Balozi wa Tanzania nchini Burundi, DK. Jilly Maleko, na Balozi mdogo wa Burundi nchini, Kabura Cyriaque na wataalamu wa madini kutoka nchi zote mbili.

Balozi Maleko alisema Tanzania na Burundi zimekuwa zikishirikiana katika maeneo mbalimbali, ikiwamo kisiasa kiuchumi na kiutamaduni hivyo serikali imeona vyema pia kuongeza fursa ya rasilimali ya madini.

"Tanzania ina madini mengi ya kutosha na Burundi pia, kwa hiyo tutaangalia namna ya kuongeza thamani kwa pamoja na kuuza katika soko la nje,'' alisema.

Naye, Balozi mdogo wa Burundi nchini, Kabura Cyriaque, alisema anaamini maazimio ya kikao hicho yatakuwa na matunda yenye manufaa kwa hizo nchi mbili.

"Ushirikiano huu unakwenda kuzisaidia nchi hizi mbili kupata maendeleo tofauti na awali," alisema.

# Operesheni ya ujangili yanasa silaha 126 Arusha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha, kwa kushirikiana na Kikosi cha Kudhibiti Ujangili Kanda ya Kaskazini (KDU), chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), wamekamata silaha 126 zilizotumika kwenye matukio ya uhalifu ya wanyamapori kwa kipindi cha miaka 10.

Akizungumza na vyombo vya habari jana jijini Arusha, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, ACP Salumu Hamduni, alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama vilikamata silaha hizo zikihusika kwenye matukio ya kiuhalifu ya wanyamapori.

Alisema kati ya silaha hizo 126, magobore ni 125 na Semi-Automatic Rifle ni moja na zilihusika kwenye matukio ya wanyamapori.

Alisema baada ya utaratibu wa kisheria kukamilika silaha zote zinatarajiwa kupelekwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya utaratibu wa kuziteketeza ili zisiweze kuendelea kwenye shughuli za kihalifu kwenye mtandao wa majangili.

"Natoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za uhalifu kwa Jeshi la Polisi, kikosi kudhibiti ujangili na vyombo vingine vya usalama ili kuwafichua wahalifu wanaojihusisha na ujangili na hata katika hifadhi bila utaratibu," alisema.

Katika tukio lingine Jeshi la Polisi mkoani humo, linamshikilia Mbise Lukumo (30), kwa tuhuma za kuhusika na kifo cha Anna Edward (44), mkazi wa Mtaa wa Kona ya A TO Z, Kata ya Matevezi Halmashauri ya Jiji la Arusha.

"Ndugu wanahabari kama mnakumbuka Januari 25, mwaka huu, liliripotiwa tukio la mwanamke mmoja aliyetambulika Anna Edward mkazi wa mtaa wa Kona ya A TO Z Kata ya Matevezi jijini Arusha," alisema na kuongeza:

"Tukio hilo lilisababisha baadhi ya wanawake kuandamana na kufunga barabara Januari 30, mwaka huu, ikiwa ni njia ya kufikisha malalamiko yao kwa serikali na hali hiyo ilinilazimu niongee nao kuomba muda wa kufanyia kazi malalamiko yao ya tukio la mauaji."

Kamanda Hamduni alisema Januari 27 majira ya saa 9:30 kikosi cha askari polisi kilimkamata mtuhumiwa Mbise Lekumo, mkazi wa Olasiti jijini Arusha, na baada ya kumuhoji alikiri kuhusika na tukio la mauaji pamoja na matukio mengine.

Aidha, alisema tukio la kwanza lilitokea Mei 21, 2019, eneo la Lolovono katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, na mtuhumiwa alikiri kushirikiana na wenzake kumuua mwanamke aliyetambulika kwa jina la Stella Daniel na katika tukio lingine Januari 16, mwaka huu, eneo la Ngaramtoni ya Chini mtuhumiwa na wenzake walishirikiana kumuua Bahati Prosper (35).

Alisema kumuhoji mtuhumiwa aliwataja wenzake walioshirikiana naye kuwa ni Lembeka Olomorojo (62), mkazi wa Olositi jijini Arusha na Bashiri Msuya (64), mganga wa kienyeji na mkazi wa Mtaa wa Kidika B, Kata ya Osunyai jijini Arusha na chanzo cha tukio hilo inadaiwa ni imani za kishirikina.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Nippo, wakiendelea na ujenzi wa barabara ya Bagamoyo kutoka Mwenge hadi Morocco jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 17 mbaroni kwa makosa ya jinai

**Elizabeth Faustine na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza, linawashikilia watuhumiwa 17 wa makosa mbalimbali ikiwamo mauaji ya familia, ubakaji, ukatili wa kijinsia, uporaji na utengenezaji wa pombe haramu aina ya gongo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, alisema hatua hiyo inafuatia msako mkali uliofanywa na jeshi hilo kuanzia Januari mosi hada Februari 16, mwaka 2021 na kufanikiwa kukamata gari aina ya Toyota Harrier namba T121 DHE ambalo limewekewa 'chesses' na namba za usajili wa gari nyingine.

Vifaa vingine vilivyokamatwa ni pamoja na pikipiki 6, runinga 10, sabufa 4, simu za mkononi 51, mitambo 7 ya kutengenezea pombe aina ya gongo, pombe lita 100, bangi kg 100, mirungi kilo 30 na kompyuta 2.

"Kufuatia msako huo mkali wa kata kwa kata, mtaa kwa mtaa ninahakikisha tunanaongozwa na intelijensia ya jinai ili kuhakikisha hatukosei mtu, lakini tunahakikisha tunapata sapoti ya wananchi kwenye ushahidi dhidi ya watu mbalimbali waliofanya makosa hayo," alifafanua Muliro.

Kamanda Muliro aliwataja watuhumiwa hao ni Bakari Hamiss (21) mkazi wa mtaa wa Mlimani B anayejihusisha na matukio ya mauaji, John Ezekiel (25) Amosi Lucas (19), Daniel Mussa (24) wakazi wa Kayenze watuhumiwa wa makosa ya ubakaji, Said Yusufu (24) Said Ramadhani (27) Hamisi Hussein (60) na Shaban Sarehe (9) wanaokabiliwa na makosa ya ubakaji.

Aidha, katika hatua nyingine Kamanda Muliro alitoa tahadhari kwa wamiliki wa magari na madereva ambao magari yao yanadaiwa faini kutokana makosa mbalimbali ya usalama barabarani ambapo magari 510 yalikamatwa kutokana na makosa mbalimbali.

"Natoa wito hii haitakuwa na msamaria mtume, hizo faini ambazo zimetozwa kisheria baada ya wao kufanya makosa ni pesa ya serikali tusije tukalaumiana katika hili, magari yote ambayo yametozwa faini hii wao wenyewe wakalipe kabla ya msako mkali ambao umeshaanza," alisema Muliro.

HABARI KITAIFA

## Bil. 40/- kujenga makao makuu ya Posta Afrika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UMOJA wa Mashirika ya Posta Afrika (PAPU), unatarajia kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu yake jijini Arusha, Machi, 2022 ambao unagharimu Sh. bilioni 40.7.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kutembelewa na Katibu Mkuu wa Umoja huo.

Dk. Ndugulile alisema ujenzi wake umeshaanza na unatarajiwa kukamilika Machi mwakani.

"Pamoja na kuwa makao makuu ya Posta Afrika yalikuwa jijini Arusha hapa nchini, bado tulikuwa hatuna jengo, lakini sasa Tanzania tumetoa kiwanja na shirika limetoa fedha kwa ajili ya ujenzi huu," alifafanua Dk. Ndugulile

Pia Dk. Ndugulile alisema kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo la makao makuu ya Posta Afrika kutasaidia kutimia kwa maono ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ambaye ndiye alihusika katika uwepo wa makao makuu ya Shirika la Posta Tanzania.

"Kama ambavyo mnafahamu kuwa Arusha ndiyo Geneva ya Afrika zipo ofisi nyingi pale za kimataifa pamoja na hii ya Posta Afrika, lakini ipo mahakama ya haki za binadamu, Mahakama ya Rwanda na nyingine nyingi," alisema Dk. Ndugulile.

Akizungumzia utendaji wa Shirika la Posta nchini, alisema wameshaanza kufanya maboresho makubwa ikiwamo katika mifumo, mwonekano na huduma zote zitaanza kutolewa kidijitali.

"Tunataka hivi sasa mambo yabadilike kwendana na mabadiliko ya teknolojia mtu akituma barua imfikie mlengwa ndani ya siku mbili sio kama ilivyo sasa hadi wiki moja mtu anakuwa bado hajapata barua yake," alisema.

Vilevile, alisema kuwa kutokana na mabadiliko ya teknolojia kuathiri utoaji huduma wa shirika hilo hivi sasa wanataka kujikita katika kutoa huduma ya soko mtandao kwa watu kutuma na kuagiza bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

Katibu Mkuu wa Umoja huo, Younouss Djibrine, alishukuru serikali ya Tanzania kwa kuwapa ushirikano katika kuhakikisha jengo la makao makuu ya Posta Afrika linajengwa.

# Ummy: NEMC msifanye kazi za polisi

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

SERIKALI kamwe haitakuwa kikwazo kwa wawekezaji katika kutoa vibali vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira katika kuwezesha uwekezaji na maendeleo ya viwanda.

Vilevile, imelitaka Baraza la Taifa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuacha kufanya kazi kama Jeshi la Polisi na kutumia busara katika kufanya uamuzi wa kufunga viwanda.

Kauli hii ilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano ana Mazingira), Ummy Mwalimu, baada ya kufanya ziara ya kikazi katika Mkoa wa Pwani kwa lengo la kukagua shughuli za utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha inaweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na kutoa miongozo katika hifadhi ya mazingira na kuiagiza NEMC kutoa ushauri wa kitaalamu kuwezesha wawekezaji kuzingatia sheria.

"NEMC simamieni Sheria ya Mazingira, viwanda visiwe sehemu ya uchafuzi wa mazingira ili maendeleo ya viwanda yaendane na hifadhi ya mazingira.

"NEMC msifanye kazi ya polisi kwa kufunga viwanda na kutoza faini kubwa. Kaeni na wenye viwanda, waelekezeni kuzingatia sheria," aliagiza. Waziri Ummy alimwagiza Mkurugenzi wa Mji wa Kibaha kuhakikisha katika mipango na bajeti, wanatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa dampo la kisasa pamoja na kutoa elimu kwa wananchi namna bora ya kutenganisha taka kuanzia ngazi ya kaya.

"Mkurugenzi, taka ni mali, si kila taka ziende dampo, wekeni utaratibu kwenye vizimba kwa kutenganisha taka za plastiki. Taka za majumbani na taka zinazoweza kurejelezeka ili wenye viwanda vya plastiki na vile vya kutengeneza mbolea waweze kupata malighafi," aliagiza.

Akimkaribisha waziri huyo katika Mkoa wa Pwani, Mkuu wa Mkoa huo, Evarist Ndikilo, alisema unakabiliwa na tatizo la ukataji miti kutokana na matumizi ya kuni na mkaa na kutoa rai kwa wizara kuangalia uwezekano wa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwamo gesi.

Pia alishauri kuwekwa kwa utaratibu kwa wachimbaji wa mchanga, kuhakikisha kunakuwa na urejelezaji wa maeneo ya machimbo kwa kupanda miti ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

Waziri Ummy alisisitiza kuwa agenda ya mazingira ni suala mtambuka na kutoa rai kwa uongozi wa Mkoa wa Pwani kutumia sheria ndogo za halmashauri kusimamia suala la upandaji miti kwa kuanzisha vitalu vya miche.

Katika siku ya kwanza ya ziara ya Waziri Ummy Mkoa wa Pwani jana, alitembelea Dampo la Mji wa Kibaha, Kiwanda cha Futan Mining kinachojihusisha na uchenjuaji wa madini ya kopa na Kiwanda cha Prance International Ltd.



Ofisa Habari wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Kanda ya Mashariki, Zainabu Ally (katikati), akipata maelezo kwa mwandishi wa habari mwandamizi wa gazeti la Nipashe, Salome Kitomari, ya jinsi gazeti hilo linavyoandaliwa, alipotembelea chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Jenerali Mabeyo asisitiza ushirikiano vyombo vya ulinzi

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Venance Mabeyo, amevitaka vyombo vya ulinzi wa usalama kuendeleza mshikamano na ushirikiano uliopo ambao umesaidia kujenga imani kubwa kwa wananchi na kuimarisha ulinzi wa nchi.

Alisema panapo kuwapo mshikamano kunawafanya wananchi wawe na imani kubwa kwao na kuwaunga mkono.

Jenerali Mabeyo alisema hayo jana alipofika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora akiwa ziarani mkoani hapa.

Alisema katika hali iliyopo ya sasa ulimwenguni, vyombo vya ulinzi na usalama vinatakiwa kuwa na ushirikiano kwa ajili ya kukabiliana na mtu yeyote toka ndani na nje mwenye nia mbaya.

"Adui wa sasa anaweza asijitokeze moja moja kwa moja, bali anaweza kuwa miongoni mwenu, hivyo ushirikiano wa vyombo vya ulinzi na usalama ni jambo muhimu katika kuendelea kudumisha amani na utulivu nchini," alisisitiza.

Jenerali Mabeyo aliwataka vyombo vya ulinzi na usalama waliopo katika ngazi za chini kuendelea kuimarisha ushirikiano kama wanavyofanya kwa ngazi ya kitaifa.

Alisema kwa ngazi ya Taifa kila wakati wanashirikiana na wapo pamoja katika utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, Jenerali Mabeyo aliwashukuru Watanzania kwa utulivu wa hali ya juu waliouonyesha wakati uchaguzi mkuu uliopita.

Alisema hali ilitokana imani kubwa ambayo wananchi wanayo kwa vyombo vyao vya ulinzi na usalama katika kulinda amani na usalama wa nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, alisema wameanzisha utaratibu wa kukutana kila mwisho mwezi kwa vyombo vote vya ulinzi na usalama mkoani humo kwa lengo la kujenga umoja.

Alisema kuwa katika kufanikisha hilo, wanafanya mazoezi ya pamoja na kujadiliana ikiwa ni sehemu ya kuwa kitu kimoja.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ikemee kufungasha vyakula kwenye makaratasi

**KARATASI** chafu au vipande vya karatasi zinazotumiwa ofisini pamoja na magazeti yaliyosomwa ndani na nje ya nchi yamekuwa vifungashio vya vyakula yakitumiwa na wafanyabiashara kuanzia wanaouza kitoweo hadi vitafunio.

Si habari njema, kwani vipande vya magazeti haya vimepita kwenye mikono ya wengi kuanzia ughaibuni, ndani ya vyombo vya usafiri hadi nchini ambako yemepimwa kwenye mizani na kusambazwa kwa wafanyabiashara hao kabla ya kufikia wateja.

Pamoja na serikali kupiga marufuku matumizi ya vifungashio vya nailoni hasa mifuko myeusi na myeupe, bado ina wajibu wa kulinda afya za walaji kwa kukagua vifungashio vya vyakula hasa vipande vya makaratasi machafu na magazeti ili kuepusha maradhi.

Tunaipongeza kwa kusimamia kikamilifu na kutokomeza pombe za viroba na mifuko mepesi ya nailoni iliyokuwa imesambaa Tanzania nzima, kwa kuwa vyote hivyo vilikuwa kitisho kwa afya ya watu na mazingira.

Kama ambavyo wataalamu wanaeleza kuwa mifuko hiyo haikustahili kufungashia vyakula vya binadamu, tena ikidaiwa kuwa na kemikali zenye sumu zinazoweza kusababisha saratani, hata karatasi zinazotumiwa leo kufunga chapati, vitumbua, samaki wa kukaanga na nyama mabuchani pengine si salama.

Kama ambavyo mifuko ya nailoni ilivyochafua mazingira na kudhuru afya, vivyo hivyo vifungashio vya magazeti yaliyosomwa Ulaya, Amerika na China pamoja na yale yanayotumika kuzalisha karatasi laini (toilet papers) si salama na huenda likawa tishio jipya la afya za Watanzania. Ndiyo maana tunaliomba Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) kuangalia suala hilo.

Tunaona kuwa vifungashio hivyo vimepitia kwenye mikono ya wengi na hata kwenye mazingira ambayo si salama, inakuwaje yawekee vyakula?

Pengine ni wakati wa NEMC na Mamlaka ya Dawa na Chakula kuchunguza ufungashaji wa vyakula kwenye makaratasi na kutoa maelekezo. Nasi tujiulize, karatasi hizi zina usalama gani?

Mathalani, mihogo inapofungwa kwa karatasi pengine jekundu, wekundu hubaki kwenye chakula hicho. Lakini, rangi nyeusi ya maandishi huyeyushwa na mafuta ya vitafunwa hivyo na kujikamata kwenye vyakula hivyo ambavyo huliwa bila kujali chochote.

Kwenye nyama, kwa vile baadhi ya bucha hazina vifungashio wauza nyama huzifungasha kwenye magazeti, matokeo yake nyama mbichi huyeyusha makaratasi na kujaza vipande vya magazeti kwenye kitoweo hicho.


Matokeo yake nyama hupikwa na karatasi na kuongeza athari zaidi kwa kuwa kemikali zinazotumiwa kutengeneza rangi hizo zimekuwa supu na kuliwa na familia wakiwamo watoto wadogo jambo ambalo linaweza kuwa na athari zaidi.

Hili ni suala la usalama kwanza, ndiyo maana tunaomba serikali iingilie kati na kutoa mwongozo. Kama ilivyopiga marufuku kunywa pombe za viroba na kutumia mifuko ya nailoni ya viwango duni ikataze kufunga vyakula na makaratasi machafu na magazeti ambayo hayafahamiki hali ya usafi wake.

Wataalamu wa afya na mamlaka za kusimamia chakula waisaidie kudhibiti na kulinda afya za Watanzania kwa kuwa gharama ya kutibu itaendelea kuwa kubwa iwapo visababishi vya magonjwa pamoja na maradhi hayo yataachiwa kusambaa.

Aidha, kwa vile inaonekana karatasi zinafaa kuwa vifungashio na pengine hazina gharama kubwa, ni vyema serikali ikaruhusu kuwapo kwa viwanda vya kuzalisha karatasi mahsusi na zenye viwango kwa ajili ya vifungashio ili wenye uwezo wa kutumia karatasi watumie na kufunganya chakula kwa usafi na salama kulinda afya za wateja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kero wananchi kusubiri viongozi wa kitaifa, watendaji wa chini mko wapi?

Na Sabato Kasika

**WAZIRI** Mkuu, Kassim Majaliwa, hivi karibuni amewakumbusha watendaji wa serikali kuwafikia wananchi, kuwasikiliza na kutatua kero zinazowakabili, akisisitiza uwajibikaji na utumishi unaojali watu.

Akifungua Bunge Novemba mwaka jana jijini Dodoma, anasema, viongozi na watendaji wawajibike kwa wananchi badala ya kusubiri ziara za viongozi wa kitaifa na kuwataka kupanga utaratibu wa kusikiliza kero za wananchi na kuwatembelea ili kutatua migogoro inayowakabili, kwa kuwa viongozi wote wa serikali wanapimwa kwa utendaji wao.

Utatuzi wa kero za wananchi kusubiri ziara za viongozi wa kitaifa ni kero kutokana na ukweli kwamba watendaji wa ngazi za chini wapo na swali huwa wanakwama wapi? Si vyema wananchi kuonyesha mabango yenye ujumbe wa kero zao ambazo wakati mwingine zingeweza kutatuliwa katika ngazi ya chini, lakini kwa nini wasubiri ziara za viongozi wa kitaifa?

Je, wananchi kuchukua hatua hizo hawajui sehemu ya kuzipeleka? Viongozi na watendaji wa maeneo husika hawatimizi wajibu wao inavyotakiwa, au kuna vikwazo wanakutana navyo ni vipi?

Wakati mwingine inawezekana matatizo yao yako juu ya uwezo wa viongozi na watendaji wa ngazi za chini. Lakini hapo siyo mwisho, bado wana nafasi kwenda ngazi nyingine badala ya kuruka hadi kwa viongozi wa kitaifa.

Hatua ya Waziri Mkuu kuwakumbusha kutatua kero za wananchi inaashiria kuwa kuna tatizo kwa viongozi na watendaji za chini, hivyo wasiendelee kusubiri ziara za viongozi wakuu.

Viongozi wa ngazi za chini, watendaji ni vyema wahakikishe kero za wananchi wao zinatatuliwa, hasa ikiwa ni pamoja na kuitisha mikutano ya kuwasikiliza, kuwa wana mamlaka zote za kuwasimamia.

Kuwafuata wananchi na kufanya mikutano maalum ya kuzungumza na kusikiliza kero zao na kutatua zile ambazo ziko ndani ya uwezo wao, hakutakuwa na mabango ya malalamiko katika viongozi wa kitaifa.

Wakati mwingine, inawezekana migogoro mingi na kero za wananchi vinasababishwa na kutowajibika kwa baadhi ya watendaji ambao wamepewa dhamana ya kuwaongoza na kuwashirikisha katika shughuli za maendeleo.

Ikumbukwe, kutotatua kero za wananchi katika ngazi za nchini ikiwamo serikali za mitaa ni sawa na kutowatumikia vyema na hivyo wanadhani sehemu pekee ya kupeleka kero zao ni kwa viongozi wa ngazi ya kitaifa.

Watendaji na viongozi wengine wa ngazi za chini, ambao wanashindwa kumaliza matatizo, hivyo wakumbushwe kuwa madhumuni ya kuwapo kwa serikali za mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi na vyombo vya serikali za mitaa vina haki na mamlaka ya kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mpango wa shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika serikali zao na kwa taifa.

Hivyo suala la viongozi hao kutembelea maeneo yao ya kazi ili kutatua kero za wananchi ni la muhimu, kwa kuwa wakifanya hivyo, hakutakuwa na mabango yenye ujumbe wa kero zao katika mikutano ya viongozi wa kitaifa.

Zipo kero kubwa zinazotatuliwa na viongozi wa kitaifa, lakini siyo ndogo ambazo ziko ndani ya mamlaka ya watendaji, ambazo wanaweza kuzitatua wenyewe kwenye ngazi za chini.

Serikali imeweka utaratibu wa kiutawala kwa kila ngazi, kwa lengo la kutatua kero mbalimbali ili kuwafanya wananchi wawaamini, hasa kwa kuitisha mikutano ya kisheria ya mitaa na kata na kusoma taarifa za mapato na matumizi ya miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Hivyo viongozi wa ngazi ya chini wakiwamo watendaji wa mitaa na kata wakijenga utamaduni wa kuwatembelea wananchi na kusikiliza kero zinazowakabili itawasaidia kuzitafutia ufumbuzi.

Kero ndogondogo zitatuliwe na viongozi wa ngazi husika huku zile kubwa zikiachiwa viongozi wa kitaifa, na kila mtu akifanya kazi kwa nafasi yake, wananchi watapata huduma bora na zenye viwango.

Kimsingi, viongozi na watendaji ndiyo injini ya maendeleo katika maeneo yao wanayoongoza, hivyo wana dhamana ya kusimamia maendeleo na kushughulikia shida za wananchi na kujijengea uaminifu kwao, wafahamu kuwa kila kiongozi atatimiza wajibu wake itakuwa rahisi kumaliza matatizo hayo badala ya kuwa watengeneza kero na kusababisha wasiaminiwe na wale wanaowaongoza.

HABARI KITAIFA

# RC aipa neno TRA ulipaji kodi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameishauri Mamlaka ya Mapato (TRA) kufanya utaratibu wa kuingiza mtaala wa somo la kodi na maendeleo kuanzia elimu ya sekondari hadi vyuo vikuu nchini, ili kukuza uzalendo wa kulipa kodi kwa hiari.

Chalamila aliyasema hayo jana alipozungumza na uongozi wa TRA makao makuu na Mkoa wa Mbeya kufuatia kuanza kwa kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango.

Alisema uwapo wa mtaala huo utasaidia kuzalisha vijana wazalendo ambao watakuwa mstari wa mbele kulipa kodi kulingana na shughuli mbalimbali za kiuchumi na hivyo kuchochea ukuaji wa miradi ya maendeleo na hatimaye taifa kupiga hatua kutokana na kodi za wananchi.

"Mkoa wa Mbeya wafanyabiashara wana kasumba ya kukwepa kulipa kodi pamoja na matumizi ya EFD. Sasa, ili kufanikiwa, washirikisheni madiwani wakati wa kutoa elimu, watawasilisha kwenye vikao vya mabaraza ya madiwani, jambo ambalo litawasaidia kufikia malengo kwa elimu kuwafikia wananchi na kulipa kodi kwa hiari," alisema.

Chalamila alisifu elimu hiyo kutolewa wilayani Chunya ambako alidai kuna tatizo la utoroshaji wa madini, jambo ambalo pia linachangia upotevu wa mapato ya nchi.

Ofisa Kodi Mkuu, Elimu kwa Mlipakodi wa TRA Makao Makuu, James Ntalika, alisema wazo la kuanza kwa mtaala litaliwasilishwa makao makuu kwa kuwa ni jambo jema ambalo litachochea ulipaji wa kodi kwa hiari.



Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, akijibu baadhi ya kero za wananchi wa Kata ya Olasiti jijini humo jana, akiwa katika ziara yake ya kikazi ya mtaa kwa mtaa. Kulia ni Katibu Mwenezi wa CCM, wilaya ya Arusha, Denis Mwita. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Tume ya Umwagiliaji kufanyiwa maboresho

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amesema wizara yake inapitia upya utendaji kazi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili kufanya mabadiliko makubwa.

Moja ya mambo yatakayofanyiwa maboresho ni kutafuta watumishi wenye weledi wa kubuni na kusimamia miradi yenye kutoa tija kwa wakulima.

Prof. Mkenda alisema hayo wilayani Mvomero mkoani Morogoro katika ziara yake ya kukagua miradi ya maji na hali ya uzalishaji wa sukari kwenye kiwanda cha sukari cha Mtibwa na kuzungumza na wakulima wa nje wa zao hilo.

"Suala la umwagiliaji bado lina shida, tunahitaji kulipatia suluhu kwa kupitia utendaji kazi wa Tume ya Umwagiliaji mapema, kwani haiwezekani serikali ijenge miundombinu halafu uzalishaji uwe na tija ndogo, na wakati mwingine wakulima washindwe kutunza miundombinu kama kulipia umeme," alisema Prof. Mkenda.

Alisema ili kuleta ufanisi kupitia sekta ya umwagiliaji, ni lazima kufanyika kwa mabadiliko hayo ambayo yatasaidia sekta ya kilimo ikiwamo kuongeza uzalishaji katika kilimo cha miwa, ambapo kwa sasa serikali imekusudia kupunguza upungufu wa sukari nchini.

Aliutaka uongozi wa Wilaya ya Mvomero kuendelea kusimamia kazi za kilimo, ikiwamo miradi ya umwagiliaji ili wakulima waongeze tija na kulima zaidi ya mara moja kutokana na wilaya hiyo kuwa na maeneo mazuri kwa umwagiliaji.

Akizungumza kuhusu sekta ya sukari Waziri Mkenda alisema tayari mkakati wa kuona uzalishaji sukari unaongezeka umeanza kwa kuwataka wawekezaji kutumia fursa ya kilimo cha umwagiliaji kukuza tija na kutumia mbegu bora za miwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Albinus Mgonya, alisema wilaya ina eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji hekta 77,005 kati yake hekta 30,802 zinalimwa, na kuiomba wizara isaidie uanzishwaji wa miradi mingi ya umwagiliaji.

# Mvua ilivyoathiri bajeti ya TARURA

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAKALA wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Kagera, umesema unaathiriwa na mvua nyingi zinazonyesha kwa misimu miwili, licha ya bajeti ya ujenzi na ukarabati wa barabara kufika kwa wakati.

Mratibu wa TARURA Mkoa Kagera, Mhandisi Avit Theodori, ndiye aliyebainisha hayo katika mahojiano na Nipashe, na kueleza kuwa kikwazo hicho kinaifanya TARURA kubadili bajeti iliyopangwa badala yake kuielekeza kwenye maeneo ambayo yameathiriwa na mvua na kukata mawasiliano ya barabara, hivyo kuwaathiri wananchi.

"Hali hiyo inasababisha kupunguza bajeti iliyopangwa na kuielekeza katika maeneo yanayoonekana kuharibiwa na maji," alisema.

Theodori alisema, hali hiyo inasababisha kupunguza baadhi ya kilomita za matengenezo ya barabara na kwenda kutengeneza maeneo yanayoharibiwa na mvua.

"Kuongeza au kupunguza ni kutokana na mvua nyingi za misimu miwili zilizoathiri maeneo hayo muhimu... lazima zitengenezwe kwa kupunguza kilomita kwenye maeneo yaliyopangiwa na kupeleka kwenye tatizo kubwa," alisema Theodori. Alisema maeneo yanayoathiriwa ni wilaya za Bukoba na Missenyi.

Alisema kwa mwaka 20/21 TARURA Mkoa wa Kagera ilipokea Sh. bilioni 9.3 kwa ajili ya kilomita 1,580 ambazo imeshaanza kuzifanyiwa utekelezaji kwa asilimia 40.

Alisema urefu huo umeangalia ujenzi wa barabara za changarawe na udongo, barabara za lami pamoja na matengenezo kwa maeneo ya miji ndani ya wilaya.

Aliongeza kuwa mwaka 19/20 wakala ulifanikisha ujenzi wa kilomita 1,540 kwa bajeti ya Sh. bilioni 9.3 kwa kuweka kilomita 4.87za barabara ya lami na mitaro kilomita 2.9.

# Wajasiriamali wa senene waitwa TBS

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

WAJASIRIAMALI wanaouza senene mkoani Kagera wametakiwa kujitokeza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kupata alama ya ubora inayotolewa na shirika hilo.

Hatua hiyo inalenga kuwawezesha kupata masoko ya uhakika ya senene ndani na nje ya Tanzania.

Wito huo ulitolewa na Ofisa Udhibiti Ubora Kanda ya Ziwa, Vimcent Mabula, wakati akizungumza na wajasiriamali mbalimbali wakiwamo wauzaji mboga, senene na wakulima katika tamasha la siku tatu lililopewa jina la Senene Festival 2021 lililoanza Februari 12 hadi 14, mwaka huu.

Lengo la tamasha hilo ni kuwajengea uwezo kuhusu na namna ya kupata alama ya ubora wajasiriamali hao.

Vincent alisema bidhaa yenye alama ya ubora ya TBS huaminika na kwenda hadi nje ya nchi kutokana na kuwa na viwango vinavyokubalika.

Alifafanua kuwa kutokana na biashara ya senene kuonekana kupendwa na watumiaji wengi wa ndani na hata nje ya Mkoa wa Kagera, zinapokosa viwango kunafanya biashara hiyo kushuka thamani.

Alisema bidhaa zinapokuwa na viwango huleta ushindani sawa sokoni, huondoa mkanganyiko kuhusu bidhaa husika na ni fursa ya kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi bila vikwazo.

Aidha, alisema viwango hurahisisha biashara baina ya nchi na nchi ikiwamo kutoa uthibitisho wa ubora, usalama, kuaminika na ufanisi pamoja na kulinda afya na usalama wa walaji au watumiaji wa bidhaa husika.

Aliwataka wajasiriamali hao kuanza mchakato wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao ili waweze kufikia masoko ya ndani na nchi.

Naye mfanyabiashara wa Senene, Josephina Ansbert, aliishukuru TBS kwa kutoa mafunzo hayo kwa wajasiriamali kwani yatakuwa fursa kubwa kwao.

Alikiri kuwa kwake ilikuwa mara ya kwanza kusikia TBS na kueleza kuwa kwa sasa anaweza kuboresha senene wake katika kiwango cha kitaifa na kimataifa, hivyo ataanza mchakato wa kuthibitisha ubora wa senene zake.

# Waziri aitaka Kilombero kuongeza uzalishaji sukari

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

SERIKALI imeutaka uongozi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero kuhakikisha unaharakisha mchakato wa uwekezaji, ili kuongeza uwezo wake wa kuchakata miwa yote inayozalishwa na wakulima wadogo Bonde la Kilombero na kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa sukari.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alipozungumza na Menejimenti ya Kampuni ya Sukari Kilombero na wakulima wa miwa wa Wilaya ya Kilombero.

Prof. Mkenda pia alipata fursa ya kusikiliza taarifa ya Bodi ya Sukari iliyobainisha kuwa wastani wa tani 350,000 za miwa ya wakulima wadogo, sawa na tani 35,000 za sukari endapo zingechakatwa, kutonunuliwa na wamiliki wa viwanda vya kuchakata miwa vya Kilombero huku nchi ikiendelea kuwa na upungufu wa sukari.

"Hatuwezi kuwa mateka katika suala la uzalishaji sukari kwa kumtegemea mzalishaji mmoja. Tatizo wakulima wana miwa hainunuliwi na mwekezaji halafu nchi inaendelea kutoa vibali kwa mwekezaji kuagiza sukari nje ya nchi wakati anatakiwa kuongeza uwezo wa viwanda vyake kuchakata miwa ya wakulima," alisema.

Waziri Mkenda, akizungumza na wakulima wa miwa wa Wilaya ya Kilombero, alisikiliza kero za wakulima waliolalamikia kitendo cha mwekezaji wa kampuni hiyo kushindwa kununua miwa yote takriban tani 800,000 inayozalishwa na wakulima ili kuchakata sukari.

Alisema takwimu za uzalishaji miwa zinaonyesha wastani wa tani 350,000 hazijanunuliwa na mwekezaji, yaani Kilombero Sugar Co. Ltd, ambazo zingetosha kuzalisha sukari tani 35,000 na hivyo nchi ingeagiza nje sukari tani 5,000 pekee kati ya tani 40,000 za upungufu kwa sasa.

Kutokana na hali hiyo, Prof. Mkenda aliagiza uongozi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero kuharikisha mchakato wake wa kuongeza uwezo wa kiwanda kuchakata miwa kutoka tani 629,000 mwaka 2018/19 hadi kufikia tani 800,000 msimu huu, ili miwa yote ya wakulima wadogo inayozalishwa sasa na kukosa soko, itumike kuzalisha sukari.

Alibainisha mpango wa wizara yake kutaka suala la upungufu wa sukari kuisha, akipongeza hatua zilizochukuliwa na Rais John Magufuli alipoingia madarakani mwaka 2015 kudhibiti uagizaji sukari toka nje, ili kutoa fursa kwa wawekezaji wa ndani.

"Kabla Rais Magufuli hajaingia madarakani, nchi ilikuwa ikiagiza sukari tani 125,000 toka nje, lakini kutokana na hatua za udhibiti, serikali imefanikiwa kupunguza uagizaji wa sukari hadi wastani wa tani 40,000 mwaka 2020 ili kutoa fursa kwa viwanda vya ndani kuzalisha," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero, Balozi mstaafu Ami Mpungwe, alisema kiwanda hicho ni kielelezo kizuri cha faida ya ubinafishaji kutokana na kuongeza uwezo wa kuzalisha sukari kutoka tani 28,000 mwaka 1998 hadi tani 128,000 za sukari mwaka 2020 kwa viwanda vyote viwili (Kilombero I na Kilombero II).

Balozi Mpungwe alisema kampuni hiyo inategemea miwa ya wakulima wadogo kwa asilimia 50 kuzalisha sukari.

"Kama kuna mtu ana fikra kuwa wakulima wadogo tunawadharau, siyo kweli. Tunawategemea sana ili viwanda vyetu viendelee na sasa tunalenga kufikia kununua miwa ya wakulima asilimia 60 baada ya upanuzi wa kiwanda mwaka 2023," alisisitiza Balozi Mpungwe.

Mwenyekiti huyo alisema tayari wameanza kushawishi wabia wake kujenga kiwanda kipya kikubwa kitakachowezesha kuongeza uchakataji wa miwa yote ya wakulima, Sh. bilioni 584 zikihitaji.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho unatarajiwa kukamilika mwaka 2023 kikiwa na uwezo wa kuchakata tani 420 za miwa kwa saa tofauti na sasa ambapo kinachakata tani 220 kwa saa.

Prof. Mkenda yuko kwenye ziara ya kikazi kukagua utendaji kazi wa viwanda vya miwa vya Kilombero kwa siku mbili ambapo jana alikagua skimu ya umwagiliaji iliyoko Msolwa Ujamaa na kujionea shughuli mbalimbali zikiendelea.



Katibu wa Chama cha wenye Ulemavu wa Ngozi (TAS), Wilaya ya Kinondoni, Mkiwa Diwani (kulia), akipokea sehemu ya seti ya miwani ya macho na miwani tiba 30, baada ya kupata huduma ya vipimo kutoka kwa Mmiliki wa Neyz Optics Centre, Neema Zakaria, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wananchi kukabidhiwa nyumba za Magomeni

**Na Halfani Chusi**

WAKALA wa Majengo (TBA), umeihakikisha serikali kuwa mradi wa nyumba za Magomeni jijini Dar es Salaam, utakabidhiwa rasmi Aprili mwaka huu.

Awali, mradi huo ulipangwa kukamilika mapema Januari mwaka huu, lakini ilishindikana kutokana na kile kilichotajwa kuwa ni masuala ya kifedha ambayo sasa yamepatiwa ufumbuzi.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Msongwe, katika ziara yake kwenye mradi huo jana, alisema ameridhishwa na maelezo ya meneja mradi huo kukamilika kwa mradi huo mapema Aprili baada ya kupitia na kukagua kazi iliyofanyika.

Alisema amejiridhisha mradi huo una dalili zote za kukamilika kwa muda huo uliopangwa.

"Mradi huu ulibidi ukamilike mapema mwezi wa kwanza (Januari) mwaka huu, lakini kuna baadhi ya masuala ya kifedha yalitokea ndiyo maana ukashindwa kukamilika, lakini sasa kwa hatua hii iliyofikia na jinsi mradi nilivyooukagua, wananchi wajiandae mapema mwezi wa nne (Aprili) kuingia katika makazi mapya.

"Kwa sasa hakuna tena sababu ya mradi huo kutokakamilika mwezi wa nne kwa sababu pesa ipo. Hivyo, ni jukumu lao TBA kuhakikisha wanatukabidhi mradi ifikapo mwezi wa nne kama walivyosema," alisema.

Meneja wa Mradi huo, Benard Kayemba, alimshukuru Rais Magufuli kwa kuwapa kipaumbele na kuwaamini kutekeleza mradi huo.

Alibainisha kuwa maelekezo yote yaliyotolewa na Rais Magufuli kuhusu mradi huo yamezingatiwa.

"Tunamshukuru Rais wetu, mtetezi wa wanyonge kwa kutuamini katika mradi huu mkubwa na hatimaye tumefikia asilimia 91. Ni jambo la kushukuru na tumefanya kazi kwa moyo mmoja na kuonyesha ubunifu mkubwa katika majengo haya," alisema. Mradi huo ambao pia umetajwa kutumia zaidi ya Sh. bilioni 50, unatarajiwa kuzinufaisha kaya 456.

HABARI KITAIFA

# Kibano chaja wanaoingilia leseni za madini

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Madini imewaonya watu wanaoingilia taratibu za utoaji leseni za uchimbaji wa madini kwa kueleza kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria na watachukua hatua kali kwa atakayebainika.

Hayo yameelezwa na Ofisa Madini wa mikoa ya Simiyu na Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, katika Kongamano la wadau wa madini lililofanyika mkoani Simiyu na kujumuisha Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya tano za mkoa huo, pamoja na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama vya mkoa huo.

Kumburu alisema atakayebainika kufanya hivyo atashtakiwa yeye binafsi kwa kwenda kinyume cha sheria za madini.

Alisema Tume hiyo imesitisha kwa muda leseni kadhaa za watu waliyoomba kuchimba madini mkoani Simiyu.

"Serikali imekuwa ikishtakiwa kutokana na watu kutoa kauli ambazo zinakwenda kinyume cha taratibu za madini naomba ieleweke hivyo na sio vinginevyo."

Naye Mwanasheria wa Tume ya Madini, Khadija Ramadahini, alisema leseni za madini zinaeleza wazi watu wenye mashamba wanatakiwa kushirikishwa, lakini wachimbaji wengi wamekuwa hawazingatii hilo. "Leseni ya madini kabla ya kutolewa kifungu cha 95 kinasema kwamba kabla ya mmiliki wa leseni ajaanza kufanya chochote kwenye eneo husika anatakiwa kumshirikisha mwenye eneo na sio vinginevyo," alisema Ramadhani. Masha Ntizu, mchimbaji madini alisema ni jambo la kushangaza kuona mtu anasitisha leseni kwa maslahi yake binafsi, licha ya kutumia gharama nyingi kuomba leseni.

"Hadi mtu apate leseni anakuwa amezunguka sehemu nyingi ametumia gharama nyingi inakuwaje mtu mmoja tu tena kwa maslahi yake binafsi anakuja na kuamua kusitisha leseni, Mwanasheria tunaomba utuambie hili, maana sheria ni zile zile sio kwamba Simiyu kuna sheria tofauti?" Alihoji Ntizu.

Naye Emannuel Gungu alisema kwa sasa kilichopo ni upya wa upatikanaji wa madini, lakini siku zinavyokwenda watu wataelewa taratibu na kanuni za madini zinavyosema. Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, alitoa msimamo wa wilaya yake kwa kueleza kuwa kila mtu anayetaka kuchimba madini afuate taratibu na sheria.



Meneja wa Benki ya NMB, Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, Abel Chitojo, akitoa elimu kuhusu huduma ya bima ya ajali inayotolewa na benki hiyo, kwa vikundi vya madereva wa bodaboda, wananchi, watendaji wa vijiji na wateja, wilayani humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# 'Msako wanaotumikisha wenye ulemavu endelevu'

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu), Jenista Mhagama, amesema serikali itaendelea na kampeni ya kuwasaka na kuwakamata waliowageuza watu wenye ulemavu kuwa vitega uchumi vyao.

Mhagama aliyasema hayo wakati akipokea msaada wa miguu bandia itakayowasaidia watu wenye ulemavu kutoka kampuni ya Kamal Group ya jijini Dar es Salaam.

Zaidi ya watu 200 waliopoteza miguu yao kutokana na ajali na magonjwa wataweza kutembea tena baada ya kampuni hiyo kutoa msaada ikiwa ni zawadi ya mwaka mpya.

Akizungumza kuhusu kampeni hiyo ya kuwasaka watu hao Waziri Mhagama alisema ni endelevu.

"Tunaishukuru kampuni ya Kamal Group kwa namna mlivyoonyesha mapenzi kwa watu wenye ulemavu," alisema.

Alisema huduma hiyo ni gharama ambapo mguu mmoja unauzwa hadi Sh.600,000.

Alisema hiyo ni mara ya tatu kwa kampuni hiyo kumualika kushuhudia namna wanavyosaidia kundi hilo.

Meneja wa Uhusiano wa kampuni hiyo, Hedwick Peter, alisema miguu hiyo bandia itagawiwa kwa watu wenye ulemavu kutoka Dodoma, Iringa na Dar es Salaam.

"Idadi hii inafikisha jumla ya miguu bandia iliyotolewa na kampuni yetu kufikia 600 tangu mpango huu tulipouanzisha miaka mitano iliyopita kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi (Peoples' Empowerment Foundation (PEF)," alisema.

Naye Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, aliishukuru kampuni hiyo kwa msaada huo ambao utasaidia pia watu wenye ulemavu jijini humo na kutoa rai kwa wadau wengine kuiga.

Mavunde alisema ni huduma ambayo itawasaidia wanufaika kuendelea kuendesha shughuli za kiuchumi.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia watu wenye ulemavu, Ummy Nderiananga, alisema serikali imetenga asilimia mbili kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye ulemavu na kulitaka kundi hilo lijiandae kuipokea ili iwasaidie kujikimu kiuchumi.

# Wapata ahueni vipimo vya afya

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WAKAZI wa Kata ya Maruku katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera wameondokana na tatizo la kutembea umbali wa takriban kilomita 20 kufuata huduma za vipimo, baada ya uongozi wa halmashauri hiyo kupokea vifaa tiba.

Vifaa hivyo vina thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200, kutoka asasi ya kiraia ya AHEAD Inc. USA kupitia AHEAD Tanzania.

Akizungumza wakati wa kupokea vifaa hivyo ikiwamo Ultra Sound na mashine ya kutolea dawa za usingizi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Solomon Kimilike, alisema vimetolewa kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Maruku, ambacho pia baadhi ya majengo yake yamejengwa kwa ufadhili wa asasi hiyo.

"Baada ya kuona jitihada za asasi hii, serikali kwa kutambua mchango wao, ilitoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya kuongeza majengo na kuipandisha hadhi zahanati ya Maruku kuwa kituo cha afya, ili kupanua utoaji huduma," alisema.

Alisema halmashauri hiyo kwa kutumia mapato yake ya ndani imeshafikisha huduma ya umeme katika kituo hicho na kumwagiza mganga mkuu kumteua muuguzi atakayekwenda kupata mafunzo ya namna ya kutumia mashine ya dawa ya usingizi, ili ianze kutoa huduma kwa wananchi.

Akitoa ufafanuzi wa matumizi ya mashine ya Ultra Sound, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Bandioti Gavyole, alisema itasaidia kupima matatizo mbalimbali katika mwili wa binadamu ukiwamo uvimbe."Lakini tunalenga zaidi kuitumia kuwapima wajawazito ili kuona maendeleo ya mtoto aliyeko tumboni, na kuona kama kuna dalili zozote hatarishi, ili hatua za haraka za kuokoa maisha ya mama na mtoto ziweze kuchukuliwa," alisema.

Katibu wa AHEAD Tanzania, Thomas Ngirwa, akikabidhi vifaa hivyo alisema lengo lao ni kushirikiana na jamii kuunga mkono jitihada za serikali za kuhakikisha inatoa huduma bora kwa wananchi.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Butairuka, Kata ya Maruku, Arbogast Bandiho, alimshukuru Apolinary Ngirwa kupitia Asasi ya AHEAD Inc. USA kwa kuona kikwazo kinachowakabili wananchi wa eneo hilo kufuata huduma hizo katika Manispaa ya Bukoba kwa kusafiri kilomita 20 na kuamua kukipatia ufumbuzi.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (kushoto), akikabidhiwa zawadi kutoka kwa Mkuu wa Huduma za Benki Binafsi na Kibiashara wa Benki ya Stanbic, Omari Mtiga, kabla ya kuanza kwa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Mabinti kwenye sayansi, yaliyoratibiwa na Shirika la Vijana ThinkTank, jijini Dar es Salaam. Benki hiyo, ilichangia Sh. milioni 10 kufanikisha hafla hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Fedha za TASAF zawatoa kwenye umaskini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WALENGWA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamebainisha namna fedha za mfuko huo zilivyowatoa kwenye umaskini.

Katika ziara ya maofisa wa TASAF wilayani hapa juzi kukagua maendeleo ya wanufaika wa mfuko huo, walengwa walibainisha jinsi walivyotumia fedha hizo za ruzuku kujikwamua kiuchumi.

Ester Kulwa, mmoja wa wanufaika hao, alisema kuwa baada ya kuanza kupata fedha za TASAF 2015, Sh. 48,000 kwa mwezi, alinunua mbuzi wawili, ambao baada ya miaka michache waliongezeka na kumwinua kiuchumi.

"Fedha hizi za TASAF zimenitoa kwenye umaskini. Sasa hivi maisha yangu ni mazuri, nimejenga nyumba ya bati, zamani nilikuwa kwenye tembe. Sasa nina mbuzi watano, kondoo wanne, ng'ombe wawili na bata tisa," alisema.

Mkazi huyo wa Kijiji cha Isela wilayani hapa, aliongeza akisifu: "Tunashukuru sana TASAF kwa kutupatia fedha hizi za kunusuru kaya maskini na kuzishika sisi wanawake, sababu wangekuwa wakizishika wanaume, tusingekuwa na maendeleo maana wangezitumia kuywea pombe.

Tunaomba mwendelee kutupatia fedha hizi ili tukue zaidi kiuchumi.

Fortunata Mosha, mkazi wa Kijiji cha Iselamagazi wilayani Shinyanga, alisema baada ya kupata fedha hizo za TASAF, alinunua kondoo wawili ambao walizaliana na alipouza baadhi yao, alijenga nyumba.

Alisema kwa sasa amebakiwa na kondoo 26, huku akibainisha malengo yake ni kununua ng'ombe ambao watamsaidia kwenye shughuli za kilimo.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Happiness Shayo, alisema katika halmashauri hiyo kuna wanufaika wa mfuko huo 6,870.

Alisema kuwa utaratibu wanaoutumia ni kuwapatia elimu ya ujasiriamali kwanza kabla ya kuwapatia fedha za kujikwamua kiuchumi, ili wasizitumie vibaya na kubaki maskini.

# Sababu wakulima kutaka KACU kununua tumbaku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANACHAMA wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), wameutaka uongozi wa chama hicho kuhakikisha wananunua tumbaku msimu huu kama walivyofanya msimu uliopita kwenye zao la pamba, ili kuongeza ushindani wa masoko na kampuni zinazonunua zao hilo.

Walisema kuwa, msimu uliopita chama hicho kilinunua pamba sehemu mbalimbali mkoani Shinyanga na kusababisha kuongezeka kwa ushindani wa masoko na kampuni zinazonunuza zao hilo kutoka Sh. 800 kwa kilo hadi Sh. 920.

Walitoa rai hiyo wakati wa Mkutano wa 25 wa KACU uliojumuisha Katibu Tawala wa Mkoa, Albert Msovela, Taasisi za kifedha, Bodi ya Tumbaku na Pamba, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na wakulima wa mazao ya tumbaku na pamba kutoka Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama.

Mankenzi Nkunda, mkulima wa AMCOS ya Tujitegeme, alisema KACU kununua tumbaku, kuchakata na kuuza yenyewe kama ilivyofanya kwenye pamba itasaidia kuongezeka kwa ushindani wa kampuni ya ununuzi wa zao hilo na tumbaku inayolimwa nje ya mkataba itapata soko. Alisema msimu uliopita zaidi ya kilo 12,000 za tumbaku zilibaki kwa kukosa mnunuzi, na kampuni zilinunua tumbaku iliyokuwapo kwenye mkataba na kusababisha tumbuku hiyo kuharibika kwenye maghala na wakulima kupata hasara kwa kile walichokuwa wamekiwekeza shambani.

Naye Malia Shija, wa AMCOS ya Mweli, alisema wamekuwa wakizalisha tumbaku zaidi ya nje ya mkataba waliofunga na kampuni za ununuzi na tunapokutana mezani kununua upya tumbaku hiyo wanalazimika kuiuza kwa bei ya hasara ili isiendelee kuharibika kwenye maghala.

Joseph Nganiki, alisema kuwa, mwaka 2017/2018 wakulima wengi walipata hasara kwa kuuza zao hilo kwa bei ya chini kwa sababu ya uzalishaji ulipitiliza nje ya mikataba hivyo KACU ichukue jukumu la kununua zao hilo kwa kutumia fedha ambazo imekuwa ikikopeshwa na taasisi za kifedha.

Mwenyekiti wa KACU, Emmanuel Charahani, alisema wako mbioni kuanza kununua tumbaku kama walivyofanya msimu uliopita kwenye pamba, na sasa wako katika hatua ya kusajili kampuni ya ununuzi wa zao hilo.

Naye Meneja wa Kitengo Kilimo Biashara Makao Makuu ya Benki ya CRDB, Richard Tarimo, alisema ili wakikopeshe chama hicho fedha za ununuzi wa tumbaku, wanatakiwa kuwa na mikataba ya kununua tumbaku kwa wakulima, na wapi watauza tumbaku yao baada ya kuichakata.

# Wamachinga wahakikishiwa miundombinu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Kibaha Mjini mkoani Pwani, Musa Ndomba, amesema miundombinu katika soko la wajasiriamali wadogo Picha ya Ndege inashughulikiwa ili kuwawezesha wafanye biashara muda wote.

Ndomba alisema baada ya wafanyabiashara hao kuondoka barabarani, eneo walilohamishiwa miundombinu linatengenezwa ikiwamo umeme na maji.

Alisema wapo wafanyabiashara ambao hawajahamia katika eneo walilopangiwa watapewa barua na viongozi wa serikali ya mtaa kuwasisitiza kuondoka eneo la barabarani, ambapo kuna ujenzi unaendelea kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa.

Ndomba ambaye ni Diwani wa Sofu lilipo soko hilo, alisema anatarajia kukutana na wamiliki wa nyumba zilizopo karibu na barabarani kuacha kuwaruhusu watu kufanyika biashara kwenye vibaraza vyao badala yake wazuie ili waende kwenye soko jipya.

"Tutajipanga pia kutoa elimu kwa wafanyabiashara ambao wamekaidi kuhamia kwenye soko jipya, watambue hasara za kuendelea kubaki barabarani na faida zinapopatikana katika eneo hili jipya ambalo sio la muda tena kama wengine wanavyofikiri," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Misufini lilipo soko, Ester Mainoya, alisema wafanyabiashara waliokuwa wanagoma kuhamia eneo walilotengewa ambalo ni la Shirika la Elimu Kibaha, wengi wao wanadaiwa kuingizwa kwenye mambo ya kisiasa ya kukwamisha juhudi na sasa wameelewa umuhimu wa soko hilo.

Mwenyekiti msaidizi wa soko hilo, Daniel Athumani, alisema idadi kubwa ya wafanyabiashara wamehamia katika soko hilo baada ya uhamasishaji uliofanywa na uongozi wa mkoa na wilaya.

Mmoja wa wafanyabiashara, Hadija Hamza, alisema awali hawakuwa na uhakika na eneo jipya, lakini baada ya kuhamia katika eneo hilo, mambo yamekuwa tofauti kwani wananchi wanawafuata wenyewe kwa wingi.

Naye Loyce Singa aliishukuru serikali kwa kuwahamishia katika eneo hilo ambalo wanafanya biashara kuliko walipokuwa barabarani na kwamba wananchi wengi wameshaanza kuzoea kuwafuata.



‘WAOO NGOZI - OKONJO-IWEALA’

Ukurasa 14



Ukurasa 13

**JPM anapoweka hisia mpya ya historia, siasa ya nchi**



Ukurasa 13

**Chuo cha Nyerere Kibaha na ujio wa fikra mpya kizalendo**

siasa

JUMATANO FEBRUARI 17, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# SUK mwiba rushwa, ubadhirifu

• Kuifanya Z’bar Dubai, Singapore ya Afrika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADA ya mkwamo wa miaka mitano wa kukosekana Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar, matumaini yameanza kuonekana baada ya awamu ya nane kuunda SUK.

Hayo yanafanyika ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyeanza kuiongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Novemba mwaka jana.

Katiba ya sasa ya Zanzibar imeweka masharti ya kuundwa kwa SUK, ikielekeza kuwa chama kinachoshika nafasi ya urais kinatakiwa kushirikiana na kilichopata nafasi ya pili katika uchaguzi mkuu ikiwa kimepata kuanzia asilimia 10 ya kura kwenye matokeo ya urais ili kiweze kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Hata hivyo, mwaka 2016 Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilishindikana kuundwa baada ya chama cha CUF kususia uchaguzi wa marudio, uliofanyika kufuatia matokeo ya ule wa mwaka 2015 kufutwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, akiongozwa na Mwenyekiti Jecha Salim Jecha.

Tume ilifuta uchaguzi huo kwa maelezo mbalimbali mojawapo ikiwa ni udanganyifu, ikieleza kuwa kulikuwa na idadi ya kura iliyozidi orodha ya wapigakura waliosajiliwa vituoni.

Hata hivyo, Chama cha Wananchi CUF kiliendelea na msimamo wa kupinga hoja za Mwenyekiti wa ZEC Jecha kuhusu kuufuta.

Kwa msingi huo, CCM iliandika historia, kwani kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 ilishinda viti vyote katika majimbo 54 ya uchaguzi katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Pamoja na ushindi huo, ilivikaribisha vyama vya ADC, AFFP na ADA-TADEA kwa kuwateua kuwa wawakilishi kupitia nafasi 10 za kikatiba za Rais. Kupitia mchakato huo, Hamad Rashid Mohamed wa ADC, aliteuliwa kuwa Waziri wa Afya, Juma Ali Khatib na Saidi Soud mawaziri wasiokua na wizara maalum.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Makamu wa Kwanza wa Rais, Seif Sharrif Hamad, wakati wa kiapo cha utii baada ya makubaliano ya kuunda SUK hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

**KUREJESHA SUK 2020**

Maridhiano yamepata uzito zaidi tangu alipoapishwa Rais wa Zanzibar Novemba 2, 2020 na kuahidi kuyaendeleza na kuyalinda akisisitiza kuwa hakuna maendeleo yanayoweza kupatikana bila ya watu kuwa wamoja.

Kwa kauli hiyo, alianza juhudi za kufikia maridhiano na Chama cha ACT-Wazalendo ambacho kilikuwa na kigugumizi cha matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Nuru ya matumaini ilionekana baada ya Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharrif Hamad, kukubali kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kula kiapo cha uaminifu kwa serikali.

**MAJUKUMU**

Maalim Seif anashika wadhifa wa Makamu wa Kwanza wa Rais baada ya kuwa katika nafasi hiyo mwaka 2010 hadi 2015 na kuwa sehemu ya uongozi wa Baraza la Mapinduzi.

Mwaka huu ameingia kwenye uongozi akiwa na idadi ndogo ya mawaziri kutokana na kura chache ya kura ACT-Wazalendo walizopata majimboni.

“Maridhiano yamewaunganisha wananchi, yameondoa siasa za chuki na uhasama. Naamini hatuwezi kupiga hatua kimaendeleo bila ya kuwa na umoja. Dhamira yangu ni kuharakisha maendeleo ya Zanzibar hatutafika huko ukiongoza watu wakiwa wamegawanyika,” anasisitiza Rais Mwinyi.

Akizungumza na wanachama wake wa ACT, Maalim Seif, anasema ameamua kuingia katika serikali ya pamoja baada ya kuridhishwa na ahadi za Rais Mwinyi, kuhusu kuwaunganisha Wazanzibari na hatua anazoendelea kuchukua za kujenga utawala bora ikiwamo kupambana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.

“Wanaopinga maridhiano ni maadui wanaotaka kuturudisha nyuma kimaendeleo tusiwape nafasi. Zanzibar imeonyesha mwelekeo mzuri kwa maelewano yanayoendelea kujitokeza katika jamii na siasa za chuki na uhasama zinamalizika,” anasema Maalim Seif.

**MATARAJIO YA UMMA**

Pamoja na mafanikio yanayozungumziwa SUK inapaswa kuyaendeleza kwa vitendo matumaini waliyokuwa nayo wananchi hasa katika kuleta unafuu wa maisha, kupambana na rushwa na ufisadi kwa vitendo.

Wazanzibari wanataka kuhakikishiwa kuwa waliofanya vitendo hivyo wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria badala ya kusimamishwa bila kuchukuliwa hatua.

Msimamo wa Maalim Seif na Dk. Mwinyi unaonekana kufanana kwenye kupiga vita ubaguzi wa aina yoyote, rushwa, ubadhirifu pamoja na kufungua milango ya kiuchumi kupata wawekezaji na kuanzisha miradi mikubwa kama ya bandari na rasilimali za baharini ili kufika malengo ya kufanya Zanzibar kuwa kama jiji la Dubai au bandari huru ya Singapore.

**HISTORIA YA SUK**

Maridhiano au mwafaka wa CCM na CUF ndiyo yaliyozaa mfumo wa SUK baada ya Zanzibar kuwa na mpasuko wa kisiasa na kusababisha changamoto nyingi ikiwamo ya kupoteza maisha na wakimbizi kukimbilia nchi jirani.

Hata hivyo, wadau wa kitaifa na kimataifa ikiwamo Jumuiya ya Madola iliingilia kati na kufanikisha mwafaka uliofikiwa baina ya CUF na CCM na moja ya makubaliano yaliyoafikiwa ni kuundwa kwa serikali ya pamoja na hilo ndilo liliendelezwa katika awamu hii kudumisha umoja na mshikamano wa Zanzibar.

# JPM anapoweka hisia mpya ya historia, siasa ya nchi

• Ndalichako azindua mkakati wa ufundishaji upya siasa, historia



JPM akizindua soko la Chifu Kingalu jijini Morogoro wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

**Na Miki Tasseni**

RAIS John Magufuli, ameanzisha wimbi jingine la tafakuri ya kihistoria nchini, akiwa katika ziara mkoani Morogoro ambako alizindua soko la manispaa hiyo na kuipa jina la Chifu Kingalu. Kwa vile yuko mrithi wa sasa wa jina hilo ambaye Rais alimtambua kuwa ni chifu licha ya kuwa nafasi hiyo siyo ngazi ya utawala ila uongozi wa kijamii kama walivyo viongozi wa dini na waganga wa asili, jina la soko hilo lilikwenda kwake, ila kimsingi lilienda kwa babu yake, aliyekuwapo wakati wa ukoloni katika harakati za uhuru.

JPM alielezea michango ya Chifu Kingalu wa kabila la Waluguru katika harakati ya kutafuta uhuru, akamtaja pia Chifu Patrick Kunambi, ambaye pamoja na mkewe Bernadetta walikuwa mstari wa mbele wa kupigania uhuru na uhamasishaji hadi miaka ya 1970. Ni maeneo kama hayo ambayo JPM alitaka watu wayaenzi, siyo kwa kabila hilo tu ila kila mahali nchini, jambo ambalo kwa wanaofahamu mikondo ya utafiti kuhusu historia ya Tanzania katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wanaelewa mikasa na hatima ambako suala hilo limepitia. Ila sasa limefanuliwa kisiasa, na mkakati wa mabadiliko kutolewa.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Joyce Ndalichako baada ya maelezo ya Rais Magufuli ametoa maelekezo kwa wasimamizi wa mitaala kuandaa mwelekeo mpya wa kufundisha somo la historia. Mabadiliko yanayolengwa yanaendana na mitaala iliyopo katika maeneo kadhaa, hasa kwa ulengwa wa kupinga ukoloni na harakati tofauti za kupambana na utawala wa Ujerumani na Uingereza. Mwelekeo wa JPM na mwongozo wa waziri vinaendana na falsafa ya suala hilo kama ilivyo katika mitaala, ila kuna mpangilio mpya ambao ulishasahaulika UDSM.

> Bado kuna kitambo kidogo hadi kufikia muda wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa mwelekeo aliouita JPM na alichosema, Waziri kuhusu mtaala wa somo hilo na kuurekebisha.

Wakati kampasi kuu ya UDSM inafunguliwa mwaka 1964 ikiwa na vitivo vitatu cha sheria, elimu jamii na sayansi, mwelekeo wa utafiti katika historia ulilenga kile kinachoitwa historia za maeneo tofauti nchini, kama wakazi wa maeneo husika walivyoishi na kushuhudia. Kazi nyingi zilitayarishwa kama mada za tungo au tafiti za shahada na machapisho ya kitaaluma, hadi kuingia miaka ya 1970 mwanzoni. Wakati huo wasomii wa fikra ya kimapinduzi walikuwa wamesheheni chuoni, tofauti na nyakati za awali ambako zaidi walikuwa wenye hisia ya uhuru wa Mwafrika na mchango wake.

Hisia hiyo ya kimapinduzi iliendana na azma ya TANU ya kufifisha ukabila na kuweka mbele hisia za utaifa, uzalendo na ujamaa kama lengo la kufundisha, hivyo kuondoa utaratibu au mwelekeo wa utafiti wa 'historia ya maeneo' na badala yake kufuatilia 'harakati za kitabaka.'

Hivyo utafiti wa historia katika vyuo na hasa UDSM ukaacha kuangalia maeneo na kufuatilia zaidi shughuli, harakati au taabu za matabaka tofauti, na hasa tabaka la wakulima ambako kungekuwa na muda, au mwamko wakati huo tabaka la wanawake lingefanyiwa kazi kubwa lilifanya nini katika kipindi hicho. Kwa maana hiyo mwelekeo mpya aliotoa JPM na mkakati wa kurekebisha ufundishaji wa historia siyo tu kurekebisha walichounda wanamapinduzi na kutaka kuona maeneo yamefanya nini katika kipindi gani, wakiongozwa na watu wao huko.

Bado kuna kitambo kidogo hadi kufikia muda wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa mwelekeo aliouita JPM na alichosema, Waziri kuhusu mtaala wa somo hilo na kuurekebisha. Suala linaloweza kuangaliwa awali ni kwa kiwango gani mwelekeo wa jadi utainuliwa uanze kung'ara tena, au kutakuwa na juhudi za kuchanganya mada, ile ya maeneo halisi (makabila, yaani wilaya na mikoa) halafu historia ya harakati za kitabaka na kijinsia. Suala ni kuwa walioko shuleni leo hawana ufahamu halisi wa historia za maeneo, ni kitu kigeni kwao, na kimsingi hakileti hamasa yoyote ila harakati za wakulima na wanawake huko.

Hapo ndipo kuna mtego, kwani ilikuwa rahisi kiasi fulani kuondoa hamasa ya watafiti kutoka meeneo halisi kwenda kutafiti matabaka, yaani harakati za wakulima na baadaye matabaka ya ziada mijini na miji midogo na pia kubadili mwelekeo kutoka matabaka kwenda jinsia, yaani tabaka maalum la aina tofauti. Haitakuwa rahisi kuwaambia waache maeneo hayo ya utafiti, huku wana wenzao maeneo mengi duniani ambako 'liberalism,' uanaharakati na kupangua mapokeo ya jadi ya kijamii, inapendelea mielekeo hiyo ya kitabaka na kijinsia. Inajenga msingi halisi wa mkakati mpana wa 'haki za binadamu' kama ajenda ya kijamii na kupima uthabiti wa sera za uchumi, wakati historia za maeneo zinalenga ushiriki, uwepo, basi.

Ila inaweza kutazamiwa kuwa wafundishaji wa somo la historia katika vyuo ambao wana hisia chanya kuhusu historia ya maeneo sasa watapata nafasi ya kuwahimiza vijana wanaoinukia katika fani hiyo kuangalia sehemu ambazo wana mahusiano nayo, wayafanyie kazi. Wengi wao hawataona hiyo kuwa ni rahisi kwani hawana mizizi ya moja kwa moja na maeneo halisi, wakiwa hasa na wazazi mchanganyiko kikabila, hivyo kuwa wageni kiasi upande huu au ule.

Hata hivyo, wakati wa utafiti za maeneo halisi haikuwa lazima mtafiti atoke eneo hilo, kama hayati Profesa Isaria Kimambo alivyotafiti 'Historia ya Wapare wa Tanzania,' akiwa ni mtani na mzaliwa wa mkoa wa Kilimanjaro wanaoishi Wapare na Wachaga.

# Chuo cha Nyerere Kibaha na ujio wa fikra mpya kizalendo

Na Sabato Kasika

BABA wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere ni mashuhuri kwa fikra tunduizi (critically thinking) ambazo zimeendelea kuwaleta pamoja

Waafrika wa kona zote hasa wale aliowaunganisha kwenye harakati za kupigania uhuru wa bara hilo vuguvugu lililoanza baada ya mwaka 1961.

Nyerere anatajwa na wasomi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa na fikra tunduizi kwenye maeneo mengi na alifanya uchambuzi, kuwaza kwa kina na kutoa maamuzi na maelekezo sahihi kitaaluma, kiuchumi, kisiasa na kwenye nyanja nyingine ambayo yamekuwa na tija na yanaendelea kuishi kwa wakati wote na mojawapo ni kile alichofanya kwenye kusimamia na kuhakikisha ukombozi wa Afrika na jitihada za kuleta mtangamano wa Afrika.

Licha ya kufariki dunia miaka 22 iliyopita fikra na kazi zake zinaendelea kufanyiwa kazi na wadau hasa wana mapinduzi ndani ya CCM na Tanzania pamoja na vyama vya ukombozi vya Afrika ambao sasa wanajenga Chuo cha Uongozi cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere Kibaha kwa Mfipa mkoani Pwani, kinacholenga kutoa mafunzo ya itikadi na uongozi ili kuendeleza fikra za uzalendo na umajumuni wa Afrika, alizoziasisi.

Kazi ya kujenga chuo hicho inahusisha vyama sita vya ukombozi barani Afrika vya CCM, FRELIMO kutoka Msumbiji, ANC cha Afrika Kusini, SWAPO kutoka Namibia, wakati Zimbabwe ZANU-PF inashirika pamoja na MPLA chama kilicholeta uhuru wa Angola.

Licha ya kwamba ujenzi wa Chuo cha Uongozi cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere, unaendelea wadau wa kisiasa wakiwamo viongozi wa kisiasa, wanapokitembelea na kukagua maendeleo wanatoa maoni mbalimbali.

Miongoni mwa wadau hao walioizuru ujenzi huo ni wajumbe wa Baraza la Wadhamini wa CCM, wakiongozwa na Mwenyekiti Anna Abdallah, ambao walitembelea chuo hicho wiki iliyopita na kutoa neno kwa wanasiasa, akisema uwapo wa chuo hicho ni kuweka sehemu rasmi ambayo sasa fikra za Nyerere za kulikomboa Bara la Afrika zitatekelezwa kwa vitendo, kwa kuwa watapatikana viongozi ambao watakuwa na uzalendo wa mataifa yao.

Anna anaamini hivyo kwa kuwa mafunzo watakayopata wasomi katika chuo hicho, yataakisi na yataelekeza itikadi na falsafa za Mwalimu Nyerere ambaye alikuwa na mchango mkubwa katika ukombozi wa Afrika, uzalendo na kujitoa kwa ajili ya maendeleo ya wengine.



Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini wa CCM, Anna Abdallah (wapili kulia) na wajumbe wa baraza hilo wakipata maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

> Uzalendo humsukuma mtu kuithamini na kuionea fahari nchi yake na kuitakia mema, hivyo mzalendo ana mapenzi ya dhati kwa taifa lake na yuko tayari kulitetea.

## KUPATA MAADILI

Mwenyekiti wa baraza hilo, anawataka viongozi mbalimbali wakiwamo wa vyama vya upinzani kujiunga na chuo hicho ili kujiongezea uwezo na kujifunza maadili na uzalendo kwa nchi yao, kwa vile vyama imara kama CCM viongozi wake huandaliwa kwa njia hiyo.

"Chama kinachotaka kujiimarisha, kione umuhimu wa kuwaleta viongozi na vijana wao kupikwa hapa. Pia ninashauri kuingizwa somo la uzalendo na maadili ili wanafunzi watakaopikwa, hasa vijana wajue historia ya nchi zao," anasema.

Anaongeza kuwa Watanzania wameshuhudia hata baadhi ya watoto wa viongozi ambao wamelelewa na kuishi ndani ya CCM, wakiwa mstari wa mbele kusema mabaya kuhusu Tanzania.

"Wanaharibu taswira ya nchi hii, lakini hayo yote yataondoka iwapo watu watakuja kujifunza uzalendo katika chuo hiki, kwa sababu kiongozi mzuri anajengwa na kufundishwa uzalendo kwa taifa lake," anasema.

Mwenyekiti huyo anaeleza kuwa jina la Mwalimu Julius Nyerere limetumika katika maeneo mengi, lakini sasa anaamini kwamba, katika chuo hicho litakuwa ni eneo rasmi la kupata fikra zake za kulikomboa bara la Afrika.

"Wanafunzi watazitekeleza kwa vitendo, kwa sababu watapatikana viongozi ambao watakuwa na uzalendo kutokana na mafunzo, ndiyo maana ninashauri viongozi wakiwamo wa upinzani kutumia fursa hii kujifunza," anasema.

Makamu Mwenyekiti, Pandu Omary Kificho, anawataka vijana kujiunga na chuo hicho, ili kupata mafunzo yatakayowapa maarifa watakapofanikiwa kuwa viongozi kwenye ngazi mbalimbali.

Wakati Kificho akisema hayo, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, Rodrick Mpogolo, anasema, chuo hicho ni sehemu muhimu ya kuendeleza fikra za hayati Baba wa Taifa kwa vitendo.

Jiwe la msingi la chuo hicho, liliwekwa na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais John Magufuli, pamoja na wajumbe wa vyama sita vya ukombozi barani Afrika kwa kushirikiana na Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), akiweka jiwe hilo mwaka 2018, Rais Magufuli alikaririwa na vyombo vya habari akisema, serikali ya China na Chama cha Kikomunisti, ilitoa zaidi ya Sh. bilioni 100 kufanikisha ujenzi huo.

Mkazo wa Mwenyekiti wa CCM kuhusu chuo hicho ulikuwa ni wakati umefika wa Tanzania kutoa mafunzo ya uongozi kwa vijana wake ili waweze kuwa chachu ya maendeleo na kutetea maslahi ya nchi zao.

## UJENZI KUKAMILIKA

Msimamizi wa mradi wa ujenzi wa chuo hicho, Emanuela Kaganda, anasema ujenzi umekamilika kwenye majengo kwa gharama ya Sh. bilioni 90 na kwamba kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 200.

"Ujenzi ulianza mwaka 2018, lakini umechelewa kutokana na hali ya mvua pamoja na kuibuka kwa COVID-19. Hata hivyo tunaendelea sasa ni kupitisha rasimu ya mitaala," anasema Kaganda.

Akizungumzia hatua hiyo ya kuenzi na kudumisha uzalendo na mawazo ya kuleta maendeleo, mwanasiasa Thomas Ngawaiya, anasema uzalendo ni miongoni mwa tabia zinazochochea maendeleo ya mtu binafsi na ya nchi yake.

"Uzalendo humsukuma mtu kuithamini na kuionea fahari nchi yake na kuitakia mema, hivyo mzalendo ana mapenzi ya dhati kwa taifa lake na yuko tayari kulitetea," anasema Ngawaiya na kuongeza kuwa vijana wa siku hizi wana mihemko ya kisiasa hadi wanasahau uzalendo kwa nchi yao, hivyo Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere kinawatengeneza upya."

Anakumbusha kuwa enzi ya Baba wa Taifa, kulikuwa na vyuo vya Murutunguru, Lushoto, Hombolo na Kivukoni, vilivyowaandaa vijana kuwa viongozi kwa kuzingatia uzalendo kwa nchi yao.

"Lakini ujio wa vyama vingi vya siasa ulivifanya vikaonekana havina kazi, lakini sasa ninaamini kwamba hicho cha Kibaha kitakapoanza, kinaweza kuwa na mchango mkubwa wa kuimarisha uzalendo kwa Watanzania," anasema Ngawaiya.

# 'WAOO NGOZI - OKONJO-IWEALA'

- Mwafrika, mwanamama wa 1 kuongoza WTO
- Aibuka kidedea licha ya Trump kumkataa



Dk. Ngozi Okonjo –Eweala Mkurugenzi Mkuu wa WTO na mwanamke wa kwanza duniani kushika wadhifa huo, tangu taasisi hiyo ilipoanzishwa mwaka 1948, ikiitwa GATT lakini iliboreshwa zaidi na kuwa WTO ilipofika 1995. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

WAOO, hongera mama, ndicho kinachoendelea nchini Nigeria baada ya Dk. Ngozi Okonjo-Iweala, rasmi kutangazwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), lenye makao makuu jijini Geneva.

Dokta Ngozi Okonjo-Iweala (66), anakuwa mwanamke na Mwafrika wa kwanza kushika wadhifa huo mkubwa wa Mkurugenzi Mkuu wa shirika la biashara duniani.

Dokta Okonjo-Iweala, Novemba mwaka jana alipoonyesha nia ya kuingia WTO rais wa zamani wa Marekani Donald Trump, 'alimtusi' akamwagiza mwakilishi wake WTO Robert Lighthizer, kuzuia jina lake kuingia kwenye kinyang'anyiro hicho licha ya kwamba aliungwa mkono kwa asilimia 70 na wanachama wa WTO.

Hata hivyo, Joe Biden, alimwangusha Trump kwenye uchaguzi wa Novemba, mwaka jana na kumuunga mkono Mnigeria huyo licha ya kwamba sasa ni raia wa Marekani.

> Mama yangu ni mwanamke mwenye nguvu. Anajua namna anavyotaka mambo yafanywe na ikiwa hutafanya anavyotaka yeye, utakwama.

Okonjo-Iweala, anasema 'nina mahaba na biashara' kwa vile ndiyo inayosukumu gurudumu la maendeleo na kupandisha viwango vya maisha ya watu na kwamba hilo ndilo lililokuwa kusudi na lengo kuu la WTO, kuiona dunia inayonyanyuka na kuchipuka kupitia biashara.

Mtihani wa kwanza wa Dokta Okonjo-Iweala, unaomkabili ni mgogoro wa China na Marekani kwenye biashara ambao ulilitikisa shirika hilo na dunia tangu Trump alipoingia madarakani miaka minne iliyopita.

Tangu China ilipojiunga na WTO mwaka 2001, imekataa madai kuwa uchumi wake ni wa kibepari unaotawaliwa dola badala ya soko na unastahili kuchunguzwa na shirika hilo.

Akitoa msimamo wake anasema shirika hilo halina sababu ya kukwepa mfumo wowote wa kibiashara badala yake kinachotakiwa kufanyika ni kuangalia njia hizo na jinsi zinavyovuruga biashara na baada ya hapo shirika litumie sheria na miongozo yake kuweka mambo sawa.

"Sheria ya umadhubuti (stability), uhakika wa kinachotazamiwa (predictability) haki sawa kwa wote bila ubaguzi, uwazi vyote hivi ni kanuni na miongozo muhimu ya WTO na mfumo wa biashara duniani ndiko unakosimamia," Okonjo-Iweala, anasema kwenye mahojiano na jarida la The Africa Report , mwaka jana na kusema shirika hilo litamaliza vita na migogoro ya kibiashara iwapo litazingatia misingi hiyo.

## MITIHANI YA MKURUGENZI

Dirk Willem te Velde, mbobezi wa biashara za kimataifa jijini London anasema: "Mambo ya sasa kama nunua bidhaa za Marekani, mikakati ya Umoja wa Ulaya kuboresha biashara zake na suala la kuendelea kutoa ruzuku nchini China ni mitihani migumu kwa Mkurugenzi Mkuu wa WTO."

Anashauri kuendeleza biashara huria, kutizama masuala ya bidhaa za kiafya, chanjo na kudhibiti mabadiliko ya tabianchi na kuwa na ugunduzi zaidi, ubunifu na kutumia teknolojia ya kisasa kuwa ndiyo njia itakayolifanya shirika hilo kuwa na umuhimu wa kipekee zama hizi.

## SIFA ZA OKONJO NIGERIA

Anasifika kuwa na mbinu ya kutotaka upuuzi na kuwa makini na alionyesha umahiri katika kukabiliana na ufisadi kwenye sekta ya mafuta Nigeria ambako baadhi ya wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa hiyo kutoka nje walikuwa na nguvu na hata kuinyamazisha serikali.

Wakati akiwa Waziri wa Fedha, alipambana nao akisema wanadai pesa nyingi kama ruzuku kutoka serikalini kwa ajili ya mafuta ambayo hawakuwa wameyauza kwa vile walizoea ufisadi.

Akionyesha kuwa hataki upuuzi, wajanja walimteka mama yake, Kamene Okonjo - daktari na profesa wa sosholojia, aliwapuuza.

Mama huyo alitekwa nyara nyumbani kwake kusini mwa Nigeria mwaka 2012, wakati huo akiwa na miaka 82.

Wakati huo akiwa Waziri wa Fedha alisema waliomteka nyara mama yake kwanza walitaka ajiuzulu uwaziri, kisha wapewe fidia. Lakini alikataa kufanya yote hayo.

"Nilijua kwamba wengi wangetetea maslahi yao kwa namna yoyote ile kwa sababu walikasirishwa na hatua yangu ya kupiga vita ufisadi, baadhi yao ni wahalifu waliokuwa wauzaji wa mafuta nchini," alisema alipozungumzia tukio hilo.

Mama Okonjo aliachiwa huru ndani ya siku tano katika hali ambayo haikueleweka, lakini huenda tabia ya binti yake ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa WTO sasa ya kukataa upuuzi ilihusika katika hili.

## MAONI YA WATOTO

Mmoja wa vijana wake - Uzodinma Iweala, mwandishi wa riwaya ya 'Beast of No Nation' ya mwaka 2005, anazungumzia mama yake asivyotaka upuuzi: "Mama yangu ni mwanamke mwenye nguvu. Anajua namna anavyotaka mambo yafanywe na ikiwa hutafanya anavyotaka yeye, utakwama."

## MAMBO MAKUU YA OKONJO

Alizaliwa mwaka 1954 nchini Nigeria, amesomea Chuo Kikuu cha Harvard 1973 hadi 76 na kupata shahada ya uzamivu katika Chuo cha Teknolojia cha Massachusetts (MIT) mwaka 1981.

Alifanyakazi Benki ya Dunia kwa miaka 25 na kupanda ngazi hadi wadhifa ambao ni wa pili kiuongozi kama mkurugenzi (2007-2011).

Alikuwa Waziri wa Nigeria mara mbili mwaka 2003 hadi 2006 na 2011 mpaka 2015 akiwa mwanamke wa kwanza kushikilia wadhifa huo.

Alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa kipindi kifupi, lakini akiwa wa kwanza kushika wadhifa huo.

Ni mwanachama wa bodi za Twitter, Benki ya Standard Chartered na Shirika la Kimataifa la Ushirikiano wa Chanjo Duniani (GAVI).

Aliteuliwa na Rais Mohammadu Buhari wa Nigeria kugombea wa wadhifa wa WTO Juni 2020. **MITANDAO**



# Wasioona watahadharishwa magonjwa ya kuambukiza

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Wasioona Tanzania (TLB) Mkoa wa Dodoma, kimewataka wanachama wake kuchukua tahadhari za kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza ikiwamo Covid-19.

Tahadhari hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa huo, Omar Lubuva, alipokuwa akizungumza na wajumbe wa mkutano mkuu wa chama, jijini hapa.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa kutokana na ulemavu walionao wa kutoona wanatakiwa kuwa waangalifu katika kujilinda na magonjwa ya kuambukiza.

Aidha, aliwataka kuzingatia maelekezo ya viongozi na wataalamu wa afya yanayotolewa ikiwamo kujifukizia.

“Hapa ninaamini kila mmoja ana imani yake anayoiamini, ila ni muhimu tukamtanguliza Mungu kwa mambo yote, ikiwamo hili la hali ya hewa ya Covid -19 ili lisitukumbe, na hili linawezekana pale tutakaposhirikiana katika kujiweka kwenye mazingira yaliyo safi na kwa kufuata maelekezo,” alisema.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa chama hicho watakaochaguliwa kuwa na ubunifu wa uanzishaji wa miradi kwa ajili ya wanachama ili kuondokana na tabia ya kusubiri kufadhiliwa.

Alisema viongozi watakaochaguliwa wanatakiwa kuwa mstari wa mbele wa kuhakikisha wanakuwa na miradi yenye kuleta mabadiliko ya kiuchumi, badala ya kuwa kuona suala la kukaa na kupita mitaani kama sehemu ya kujipatia kipato cha maisha yao.

Kwa upande wake, Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu mkoani humo, Justus Ng’wantalima, aliwataka wanachama cha chama hicho cha wasioona kuungana kwa pamoja ili kupata mikopo inayotolewa ya asilimia 10 na halmashauri nchini.

Alisema wakiungana kwa pamoja watapata mikopo itakayowawezesha kuanzisha miradi mbalimbali itawaondolea dhana ya kuombaomba.



Meneja Biashara na Mkakati wa Mauzo wa Vodacom Tanzania Plc, Kanda ya Kati, Baraka Siwa, akizungumza kuhusu huduma za fedha zinazotolewa na kampuni hiyo, wakati wa mafunzo kwa waratibu wa wafanyabiashara wa huduma ndogo za fedha jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Vodacom ni mdau wa huduma za fedha kwa njia ya mtandao kupitia M-pesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# AGRA kurudisha hadhi ya masoko

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuendeleza Kilimo Afrika (AGRA) imesema itaendelea kushirikiana na serikali ili kurudisha hadhi ya masoko kwenye bidhaa za kilimo ili kuwakwamua kiuchumi wakulima na wafanyabiashara.

Makamu wa Rais wa Sera na Uwezeshaji kutoka

AGRA, Dk. Appolos Nwafor, alitoa kauli hiyo katika mkutano wa wafanyabiashara wa mazao ya

nafaka kutoka mikoa mbalimbali uliofanyika jijini hapa.

Dk. Nwafor alisema AGRA inatambua umuhimu wa masoko kwa wafanyabiashara wa mazao ya nafaka.

“AGRA ipo pamoja na serikali kuhakikisha kilimo kinapiga hatua, tunahitaji kuona pato la mfanyabiashara linaongezeka lakini pato la taifa linakuwa kiuchumi kutokana na kilimo,” alisema Nwafor.

Dk. Nwafor alisema AGRA wanatambua umuhimu wa sekta binafsi kwa wafanyabiashara wa mazao ya nafaka na kuwatoa hofu kwamba watashirikiana na serikali kufungua masoko.

Alisema watafanya juhudi kwa kushirikiana na serikali katika kurudisha hadhi ya masoko kwenye bidhaa za kilimo ili wakulima na

wafanyabiashara wafanye biashara yenye kuleta matokeo chanya. “Tupo tayari kushirikiana na serikali kuondoa vikwazo kwenye biashara mipakani lengo ni kuhakikisha pato la mkulima linaongezeka,” alisema.

Kwa upande wake, wafanyabiashara waliiomba serikali kuweka mazingira wezeshi yatakayowawezesha kufanya biashara nje ya nchi bila vikwazo vyovyote.

Daniel Medard kutoka Rusumo wilayani Ngara, alisema wamekuwa wakifanya biashara Rwanda, lakini kuna tatizo la masoko kutokana na kwamba nchini humo kuna vikundi vinavyonunua mazao kwa wafanyabiashara wa Tanzania. “Tunaomba serikali itusaidie kuweka mazingira wezeshi wafanyabiashara wa mazao ya nafaka ili tuweze kufanya biashara kiurahisi bila bughudhi,” alisema Medard.

Alisema kumekuwapo na tatizo kwenye usafirishaji ambapo ushuru umekuwa ukitozwa mara mbili mzigo unapotoka na unapokwenda jambo ambalo linampunguzia faida mfanyabiashara wa nafaka.

## Walima zabibu wapewa mbinu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Hombolo kimewataka wakulima wa zabibu kuzingatia elimu inayotolewa na wataalamu wa zao hilo, ili kuepuka kupoteza zabibu nyingi shambani msimu wa mavuno.

Hayo yalisemwa na mtafiti Andekelile Mwamahonje wakati akielezea umuhimu wa wakulima wa zao hilo linavyohitajika kuzingatia elimu ya uandaaji shamba, kupanda hadi kuvunwa wanayopewa na wataalamu wa zao hilo.

Mwamahonje alisema baadhi ya wakulima hawajui matumizi ya mbegu bora, ambapo wakishindwa kutambua hilo mwisho wa siku wanakuja kupata shida mbeleni kadri zabibu inavyoendelea kukua.

“Kuna baadhi ya hatua wakulima hawazijui ndio maana huwa tunaenda kutoa elimu kwa wakulima katika baadhi ya maeneo ili kuwasaidia wasipoteze zabibu nyingi shambani kipindi cha mavuno,” alisema Mwamahonje.

Alisema tayari walishatembelea katika halmashauri za Chamwino, Bahi, na kwingineko kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima wa zao hilo ili kuhakikisha wanafanya vizuri ifikapo msimu wa kilimo.

Alisema moja ya mikakati ya kituo hiko ni kuhakikisha wanatoa elimu kwa wakulima wa zabibu ambalo ni zao la biashara ili kuhakikisha wakulima wanafanya kilimo chenye tija.

Alisema zabibu ni zao la biashara na linapendwa na watu wengi, hivyo ni vema kila mkulima akiwa na elimu ya namna ya kutunza zao hilo tokea mwanzo wa upandaji hadi msimu wa kuvunwa.

Mwamahonje alisema wakulima wanapaswa kuzingatia maelekezo ya utunzaji kutokea msimu wa kupanda hadi mavuno kwa sababu wakifanya hivyo itawasaidia kwa kiasi kikubwa kupata mavuno mengi kipindi cha kuvunwa.

“Tunaomba wakulima wazingatie elimu inayotolewa na kituo cha utafiti wa kilimo, tunahitaji kuona wakulima wa zao hilo mkoani hapa wanapiga hatua katika kilimo hicho,” alisema Mwamahonje.

Alifafanua zaidi ya kuwa zao la zabibu halifanani na mazao mengine na inachukua muda mrefu, hivyo mkulima anapaswa kufuata taratibu ambazo watafiti wameelekeza ambazo zitawapa manufaa makubwa katika kilimo.

Naye Mary Stephene, kutoka Idara ya Mbegu, alisema kituo hicho kimekuwa kikifanya jitihada za kuhakikisha wakulima wa zao hilo mkoani hapa wanakuwa mfano wa kuigwa na wakulima wengine.

Alisema Dodoma ni mkoa pekee ambao zao hilo linalimwa msimu miwili, hivyo wakulima wanatakiwa kupata elimu mara kwa mara ya uandaaji mpaka uvunaji wa zao hilo.





# Vifaa vya mil. 824/- kuikabili saratani ya kizazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imepokea msaada wa vifaa vya kupimia saratani ya mlango wa kizazi kwenye mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 824, ili kukabiliana na ugonjwa huo, ambao unadaiwa kuwa inaongoza kugharimu maisha ya wanawake.

Vifaa hivyo vimetolewa na Shirika la Utafiti la Kimataifa la HJFMRI kupitia programu ya Walter Reed Tanzania ambapo vinatarajiwa kusambazwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya 125 vya mikoa ya Mbeya, Rukwa, Katavi na Songwe. Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Walter Reed Tanzania, Dk. David Maganga, alisema saratani ya mlango wa kizazi kwa wanawake ni tatizo kubwa nchini, na kwamba ndio maana taasisi hiyo iliamua kusaidia kupambana nao.

Alisema mwaka 2018 wanawake 6,695 nchini walibainika kuwa na viashiria vya saratani hiyo, na kwamba wanawake 22 kati ya 100,000 hufariki kila mwaka nchini kutokana na aina hiyo ya saratani.

"Saratani hii imekuwa tatizo kubwa kwa wanawake, ni aina ya saratani ambayo inaongoza kwa kuua wanawake, lakini ndiyo aina ambayo inatibika kirahisi zaidi endapo itagundulika mapema, sisi tumeamua kuungana na serikali ili kulimaliza tatizo hili," alisema Dk. Maganga.

Alisema wanawake wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (HIV) wana hatari zaidi ya kupata aina hiyo ya saratani na kwamba huwa inawaletea madhara kwa haraka zaidi kuliko wale ambao hawana maambukizi ya virusi hivyo.

Akipokea msaada huo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya, Dk. Festo Ndugange, alishukuru taasisi hiyo kwa msaada huo kwa maelezo kuwa utasaidia kukabiliana na aina hiyo ya saratani katika mikoa husika.

Aliwaomba wadau mbalimbali vikiwamo vyombo vya habari kuendelea kuhamasisha wanawake nchini kujitokeza kupima viashiria vya saratani hiyo, ili wakibainika mapema watibiwe na kuokoa maisha yao. Alisema endapo wanawake wengi watajitokeza kupima mapema aina hiyo ya saratani na kutibiwa mapema kwa wale watakaogundulika kuwa na viashiria, itasaidia hata kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na tatizo hilo nchini.

Alisema kinachotakiwa kwa Watanzania ni elimu kuhusu tatizo hilo na kwamba wakipata elimu hiyo watahamasika na kujitokeza kupima na kisha kutibiwa kwa wale wanaobainika kuwa na viashiria.

"Upimaji wa viashiria vya saratani ya mlango wa kizazi ni miongoni mwa mikakati ya serikali katika kupunguza madhara ya HIV, hivyo tunawashukuru sana Walter Reed kwa kutuunga mkono," alisema Dk. Ndugange.

Mkurugenzi wa Afya kutoka Ofisi ya Rais, Dk. Ntuli Kapologwe, alisema serikali inaendelea na mikakati ya kuimarisha afya ya msingi kwa wananchi kwa kujenga miundombinu ya kutolea huduma hizo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Mabula Mchembe (wa pili kulia), akipata maelezo ya namna Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya inavyotoa huduma kutoka kwa Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji (wa pili kushoto), alipotembelea hospitalini hapo, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TFS kugawa miche 30,000 bure

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu (TFS) kupitia shamba la miti la Kawetere lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, umeandaa miche ya miti zaidi ya 30,000 kwa ajili ya kuwagawia wananchi, taasisi za umma na vijiji vinavyozunguka shamba hilo ili kuhamasisha utunzaji wa mazingira.

Hayo yalisemwa juzi na Mhifadhi Mkuu wa Shamba hilo, Arnold Shoo, wakati wa Ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, kwenye shamba hilo iliyoambatana na kukabidhi mbao 843 kwa viongozi wa vijiji saba vya Kata ya Ihango.

Alisema wamekuwa wakiandaa miche hiyo na kuvigawia vijiji hivyo, taasisi za serikali na hata mwananchi mmoja mmoja ili wakapande kwenye maeneo yao na kusaidia kutunza mazingira ikiwamo kutokata miti ovyo.

Alisema miti ambayo wamekuwa wakiandaa ni ya mbao, kuni na ya kwenye vyanzo vya maji, na kwamba kwa sasa asilimia kubwa ya wananchi wanaoishi kuzunguka shamba hilo wamekuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa misitu.

"Hii miti tunaizalisha hapa hapa na tumekuwa tukigawa bure kwa taasisi ambazo zina uhitaji, tumewahi kugawa hata kwenye majeshi yetu na hata hawa wananchi wanaotuzunguka tumekuwa tukiwagawia bure," alisema Shoo.

Alisema shamba hilo linazungukwa na kata tisa za halmashauri tatu ambazo ni Jiji la Mbeya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya pamoja na Halmashauri ya Mbarali, na kwamba kila kata imekuwa ikinufaika na shamba hilo kwa kusaidiwa vitu mbalimbali.

Alisema kuna baadhi ya sehemu wananchi wamekuwa wakivamia msitu na kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa na hivyo akaiomba serikali kusaidia kukemea vitendo hivyo haramu. Ntinika alipongeza uongozi wa shamba hilo na kwamba wanatakiwa waendeleze ushirikiano huo na wananchi ili mazingira yaendelee kuwa salama na kuepuka mabadiliko ya tabianchi.

Alisema misitu iliyopo mkoani Mbeya ndiyo inayosababisha uwapo wa mvua ya kutosha kwa ajili ya ustawi wa mazao mbalimbali na hivyo kuufanya Mkoa huo kuwa miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula. Aliwaagiza viongozi wa vijiji vyote vinavyozunguka shamba hilo kuhakikisha wanawachukulia hatua za kisheria wananchi wanaokata miti kwa ajili ya mkaa na kwamba endapo kuna kijiji kitabainika kuna uharibifu, viongozi watawajibika.

"Nawapongeza sana TFS hapa mmetusaidia mbao ambazo zinatokana na msitu huu, sasa endeleeni kugawa miti maana wananchi wameshaanza kujua umuhimu wa misitu hii, ikiwezekana wafundisheni wananchi namna ya kuandaa miche," alisema Ntinika.

Aidha, aliwapongeza wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo kwa kusaidia kuzuia moto kwa maelezo kuwa aliambiwa kuwa kwa mwaka 2020 hakuna tukio lolote la moto lililotokea.

Aliwashauri viongozi wa mashamba mengine kujifunza utaratibu huo wa kuwashirikisha wananchi kwenye shughuli hizo za ulinzi wa mazingira.

# Mamalishe walalamikia gharama mafunzo VETA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa chakula katika Jiji la Mbeya maarufu mamalishe na baba lishe, wamelalamikia gharama kubwa ya mafunzo wanayotozwa na uongozi wa Chuo cha Ufundi Stadi Mbeya (VETA) wakidai kuwa haziendani na biashara wanazofanya.

Walitoa malalamiko hayo wakati wa kikao maalumu na Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, kilichokuwa kimelenga kusikiliza kero zao.

Mmoja wa mamalishe hao, Joyce Mwambungu, alisema ili kushiriki mafunzo hayo waliambiwa lazima walipe Sh. 25,000 ambazo kati yake Sh. 5,000 ni kwa ajili ya fomu na 20,000 inayobaki ni kwa ajili ya mafunzo, chakula na cheti.

Alisema waliambiwa kuwa mafunzo hayo ni lazima kwa kila anayefanya biashara hiyo na kwamba ambaye hatapata mafunzo hayo atazuiliwa kujishughulisha na biashara hiyo.

"Sisi biashara yetu ni ndogo na wengi tuna mitaji midogo, sasa mafunzo yenyewe ya siku moja tena saa tatu tunatozwa hela kubwa kama hii, faida ya biashara yetu ili ifikie 25,000 unaweza ukakuta umeuza zaidi ya wiki," alisema Joyce.

Akijibu malalamiko ya wafanyabiashara hao, Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Ng'wanidako alisema hata yeye haridhishwi na gharama hizo huku akiahidi kuwasiliana na Mkuu wa Chuo cha VETA ili kupata ufafanuzi wa gharama hizo.

Alisema gharama hizo hazijaainishwa vizuri kuwa mafunzo ni kiasi gani, cheti ni kiasi gani na chakula ni kiasi gani isipokuwa wameunganisha vyote bila kuwa na mchanganuo.

"Haya mafunzo yanatolewa kwa nia njema, yanalenga kuwafanya mboreshe huduma zenu, namna ya kuandaa chakula kwa kuzingatia misingi ya afya na namna ya kukifikisha kwa wateja kikiwa na hali ya usafi, lakini hizi gharama zinahitaji ufafanuzi zaidi," alisema Ng'wanidako.

Alisema kutokana na muda wa saa tatu ambao unatumika kwenye mafunzo hayo hakuna sababu ya kuweka bajeti ya chakula na badala yake washiriki wanatakiwa kwenda kula nyumbani wakimaliza mafunzo.





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, Masoud Muhammed, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Hakuna ubaguzi katika mitihani ya taifa'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAIMU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema hakubaliani na madai ya kuwapo ubaguzi wa Unguja na Pemba katika kusimamia mitihani ya taifa kwa kuwa madai hayo hayana ushahidi wowote.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi alipojibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Kombo, aliyehoji sababu za kile alichokiita ubaguzi wa Uunguja na Upemba katika kusimamia mitihani ya taifa.

Waziri Pembe alisema wasimamizi wa mitihani ya taifa huteuliwa kwa kuzingatia miongozo ya mitihani ya Baraza la Mitihani la Zanzibar na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Alisema katika miongozo hiyo, sifa za msimamizi zimeainishwa bila ya kubagua, akisisitiza kuwa mwalimu yeyote anaweza kuwa mtungaji, msimamizi na msahihishaji wa mitihani ikiwa atakidhi vigezo vilivyowekwa ikiwamo uaminifu, uadilifu na uzoefu wa kazi.

Waziri huyo pia alizungumzia kuvuja kwa mitihani ya taifa katika baadhi ya shule, akibainisha kuwa wanafunzi huadhibiwa kwa kufutiwa matokeo na waliovujisha mitihani hiyo huchukuliwa hatua.

Pembe ambaye ni Waziri wa Ardhi, alisema wanafunzi wanaobainika kufanya udanganyifu na kuthibitishwa, hufutiwa matokeo yao kwa mujibu wa kanuni za mitihani.

"Mamlaka zinazohusika kufanya uchunguzi, hutafuta aliyehusika na ikithibitika kuwa amefanya kosa hilo, sheria huchukua mkondo wake," alisema.

Waziri huyo alisema serikali inahakikisha uvujaji wa mitihani hautokei na miongoni mwa hatua inazochukua ni kutoa elimu kwa jamii ili waelewe athari za uvujishaji wa mitihani na kuweka mikakati ya kuziba mianya hiyo na kuwachukulia hatua kali za kisheria wale wote wanaobainika kuhusika na uvujaji wa mitihani.

# Waziri: Serikali haijatelekeza viwanda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema haijatelekeza maeneo huru ya uchumi ya uwekezaji yaliyopo Micheweni, Pemba ambayo lengo lake kubwa kuwakaribisha wawekezaji kuwekeza katika miradi mbalimbali ikiwamo ya viwanda.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, alitoa kauli hiyo jana alipozungumzia maeneo hayo huru ya uchumi na uwekezaji.

Alisema juhudi zimeanza kuchukuliwa katika kuyaimarisha maeneo huru ya uchumi ya Micheweni, Pemba ikiwamo kufikisha miundombinu ya barabara inayokwenda moja kwa moja katika maeneo hayo.

Alisema kazi kubwa inayofanywa kwa sasa ni kuyatangaza maeneo hayo na kuwataka wawekezaji kuwekeza huku kazi ya kuweka miundombinu ikiwamo umeme na majisafi na salama.

"Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Serikali ya Awamu ya Nane chini ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, tayari imeweka mikakati ya kuyaendeleza maeneo huru ya kiuchumi katika sera yake ya uwekezaji wa uchumi wa buluu," alisema.

Wakati huo, serikali imesema huduma zote muhimu za kijamii zinatarajiwa kufikishwa katika visiwa vidogo vilivyopo Unguja na Pemba kwa ajili ya kuwapunguzia safari za kuvuka bahari kwenda upande wa pili.

# Serikali yapeleka neema vijiji vya karibu na misitu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maliasili zisizorejesheka, imesema imeimarisha maeneo ya hifadhi ya msitu na kuweka utaratibu mzuri wa kunufaisha vijiji tisa vilivyopo jirani na maeneo hayo.

Waziri wake, Soud Nahoda, alivitaja vijiji hivyo jana kuwa ni Kitogani, Bwejuu, Pete, Michamvi, Ukongoroni, Charawe, Chwaka, Cheju na Unguja vinavyozunguka Hifadhi ya Msitu wa Jozani, Unguja.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalum, Mwanatatu Mbarouk Khamis, aliyetaka kujua faida iliyopatikana katika vijiji vilivyomo katika maeneo ya misitu ya hifadhi za taifa.

Waziri Nahoda alisema kwa vijiji vilivyonufaika kwa upande wa Pemba ambavyo vimezungukwa na msitu wa Ngezi ni Makangale, Jiwe Moja, Kijini, Tondooni, Mkia wa Ng'ombe, Bandari Kuu, Kiuyu kwa Manda, Kiuyu Kipangani, Msuka na Mjimpya.

Alisema utaratibu huo unategemewa kuendelea kwa maeneo mengine ya uhifadhi na faida iliyopatikana mpango wa faida ya utalii wa kimaumbile ambavyo wanapatiwa wanajamii wanaozunguka maeneo ya hifadhi.

Waziri huyo alisema wananchi wa maeneo hayo hufanya miradi tofauti ya kujiongezea kipato na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Alisema wanavijiji hupatiwa mafunzo ya uanzishaji wa miradi hiyo ya kujiongezea kipato ikiwamo ufugaji nyuki kibiashara, vitalu vya miche, ufugaji wa vipepeo, kilimo mseto na vitendea kazi.

"Jumla ya wanajamii 568 walipatiwa mafunzo hayo na vitendea kazi vya ufugaji nyuki vyenye thamani ya Dola za Marekani 10,181 na vitendea kazi vya uzalishaji wa miche ya msitu na matunda," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**ENEO ZURI LA KUJENGA KITUO CHA MAFUTA (PETROL STATION)**

LINAUZWA KISEMVULE BEI SHS. 500,000,000/= TU UKUBWA WA ENEO SQM 4000. TUPIGIE: 0786 302219 / 0786 306030

**ENEO LA KUJENGA KITUO CHA MAFUTA (PETROL STATION)**

LINAUZWA MBEZI NJIAPANDA YA KISIJU KILOMETA 5 KUTOKA MKURANGA. UKUBWA WA ENEO EKARI 2. PIGA SIMU: 0786 306030

**ENEO LA KUJENGA SHELL LINAUZWA MWANAGATI:**

LIpo Njiapanda ya kwenda Kilungule. Ukubwa wa eneo SQM 2,500 Bei Tshs. 450,000,000/= tu. SIMU: 0628 336736/0759 848155

**ENEO ZURI LA KUJENGA SHELL LINAUZWA TANDIKA:**

LIpo Round About ya Devis Corner. Ukubwa wa eneo SQM 2,500 Bei Tshs. 950,000,000/= SIMU: 0786 302219 / 0786 306030

**ENEO LA KUJENGA SHELL LIPO BUZA KANISANI:**

Karibu na Benki ya CRDB. Ukubwa wa eneo SQM 2500 Bei niTShs. 700,000,000/= tu. TUPIGIE SIMU: 0714 564651 / 0715 108151

**ENEO LA KUJENGA SHELL LIPO BUZA KANISANI:**

ENEO ZURI LA KUJENGA SHELL LINAUZWA TANDALE KWA M TOGOLE: Lipo Njiapanda ya Tandale Kwa Mtogole. Bei TShs. 950,000,000/= tu. TUPIGIE: 0786 302219 / 0786 306030

**NAFASI ZA SHULE**

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. M a w a s i l i a n o : 0 7 1 3 3 2 7 6 1 3 .

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI na 1 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SUBASH MOTIBHAI PATEL**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**KETAN KUMAR VINUBHAI PATEL**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**Kanuni ya 75**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu alietajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tareehe 4th mwezi MARCH mwaka 2021

Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tareehe 4th mwezi February mwaka 2021

NAIBU MSAJILI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya CHAMWINO MJINI**
**Usimamizi wa Mirathi No. 7/2021.**

Ombi la **HASSAN DACHI MAKAMBA** kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **ISMAIL DATCH MAKAMBA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 25/02/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Tarehe 16/02/2021.**

---

**MWAMBA MILLENNIUM COMPANY LIMITED**
**MNADA WA HADHARA**

**SHAURI LA MADAI NO.126/2019 KWA AMRI YA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA IRAMBA(KIOMBOI)**

Tutaendesha mnada wa hadhara wa kuuza shamba moja lililopo katika kijiji cha Songambele kata ya Ndago wilaya ya Iramba (Kiomboi) mali ya Bwana Mkoma Shilla ndani ya siku 21 ili kufidia deni analodaiwa na Bwana Abdi Hamisi, Mnada utafanyika tarehe 04.03.2021 saa tano kamili asubuhi (05:00)

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mnunuzi atalipa 25% na atamalizia ndani ya siku 14 malipo 75% ya bei itakayowekwa kwenye mnada.
3. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda uliotolewa atakuwa amepoteza haki yake.
4. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu namba **0712 245977,0654 686106,0767 245977**

**WOTE MNAKARIBISHWA**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo Mjini Morogoro**
**Usimamizi wa mirathi 44/2021**

Ombi la **RAHMA PHILIMON KAZIMOTO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **AHMAD YAHAYA MAPUNDA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **23/02/ 2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 16/02/2021**

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**PHILEMON HENRY MSEMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISH-FUSO** yenye namba za usajili **T510 CPA.** Yenye Chassis namba **FK415E521066** na Engine namba **6D14541991.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.Taarifa Polisi: **MUH/RB/492/2021.**

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**FURAHA JOHN BUKUKU** A N A T A N G A Z A KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA **NISSAN CIVILIAN BUS** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T. 611 D V K .** Y E Y O T E ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA P O L I S I **MBE/MBE/RB/90289/2021**

---

**ABA-JAJA COMPANY LIMITED**
**TAARIFA/NOTISI**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ITWANGI ILIYOPO SHINYANGA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 18/2020**
**MASANJA HAMIS (Mdai)**
**JULIUS MTATIRO & GOD FREY WAIGAMA (Wadaiwa)**
**Kwa: JULIUS MTATIRO & GODFREY WAIGAMA**

Mnataarifiwa kuwa nimepewa hati ya kukamata mali dhidi yenu katika shauri la Madai Namba 18 ya 2020 ya Mahakama ya Mwanzo Itwangi iliyopo Shinyanga. Mnataarifiwa kuwa ulipe Tsh. 2,205,000/= kwa ajili ya Mdai Masanja hamis ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi tangia siku ya kutolewa kwa taarifa (Tangazo) hili pamoja na gharama za ukazaji hukumu. Msipotekeleza hatua nyingine za ukazaji hukumu zitaendelea dhidi yenu bila taarifa (notisi) nyingine kutolewa kwenu.

C. R. Kabenga
Dalali wa Mahakama
SHINYANGA

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**HANCE JOEL MWAKANYAMALE** a n a t a n g a z a kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajii **T 992 DST – TOYOTA IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya P o l i s i : **IR/RB/1663/2020.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 53/2019**
**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA YA LINDI JINAI NA. 76/2018**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA -----MRUFANI**
**DHIDI YA**
**JUMA ALLY HAMIS @ MKULUPALILE ------MJIBU RUFANI**
**KWA:**
**JUMA LLY HAMISI @MKUKUPALILE**
**MAKONGORO**
**LINDI**

**KUITWA SHAURINI**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUDIKA MBELE YA MAHAKAMA KUUU YA MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 19/02/2021 SAA 2;30 ASUBUHI BILA KUKOSA.

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA, BASI SHAURI HILI LITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 8/2/2021.

**A.H. MSUMI**
**NAIBU MSAJILI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 33/2019**
**MKURUGENZI MASHTAKA .........................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**SALUM ABDALLAH @NALIOGO**
**ADAMU SAIDIA @OHIMBA ...........WAJIBU RUFAA**
**KWA**

1. **SALUM ABDALLLAH @NALIOGO**
   **MADIGO**
   **LINDI**
2. **ADAMU SAIDI @OHIMBA**
   **MADIGO**
   **NYANGAMALA**
   **LINDI**

**KUITWA SHAURINI**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUDIKA MBELE YA MAHAKAMA KUUU YA MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 19/02/2021 SAA 2;30 ASUBUHI BILA KUKOSA.

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA, BASI SHAURI HILI LITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 8/2/2021.

**A.H. MSUMI**
**NAIBU MSAJILI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Zuma kufunguliwa mashtaka kuidharau korti

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

MWENYEKITI wa Tume ya Uchunguzi, kuhusu madai ya rushwa yanayomkabili aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, amesema anataka kiongozi huyo ahukumiwe kifungo gerezani.

Jaji Ray Zondo alisema Zuma, alishindwa kufika mahakamani kujibu madai ya ufisadi yanayomkabili.

Jaji Zondo anamshtumu Zuma kwa kuidharau mahakama baada ya kudharau ombi la kufika mbele ya tume ya uchunguzi anayoiongoza.

Hata hivyo, Zuma alibaini kwamba mwenyekiti huyo si mtu mzuri, kwa kuwa alionyesha upendeleo katika uamuzi alioutoa dhidi yake.

Wakati huohuo, Jaji Zondo alisema yuko tayari kuomba mahakama ya juu ya Afrika Kusini, kumhukumu aliyekuwa rais kwa kosa hilo na kitendo cha kukaidi wito wa mahakama.

Mahakama ya kikatiba mwezi uliopita, ilitoa uamuzi wake na kusema kuwa Zuma analazimika kufika mbele ya tume hiyo.

Zuma anashtumiwa kuwa wakati wake madarakani, aliruhusu familia tajiri ya Gupta kupora mali ya serikali na kushawishi sera na uteuzi wa mawaziri.

Madai ambayo Zuma anaendelea kukanusha. **RFI**

## DRC yapata waziri mkuu mpya

**Kinshasa,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi amemteua mkuu wa shirika la madini kuwa waziri mkuu mpya.

Hatua hiyo ni baada ya mapambano ya muda mrefu ya kuwania madaraka na washirika wa mtangulizi wake Joseph Kabila.

Waziri Mkuu mpya, Jean-Michel Sama Lukonde Kyenge, alisema kipaumbele chake kitakuwa usalama na uthabiti katika taifa hilo linaloongoza kwa mizozo ya kivita.

Kyenge (43), ambaye uteuzi wake ulitangazwa kwenye televisheni, anachukuwa nafasi ya Sylvestre Ilunga Ilukamba, aliyelazimishwa kujiuzulu baada ya muungano kati ya wafuasi wa Tshisekedi na rais wa zamani Kabila kuvunjika.

"Usalama, kama mnavyojua ni moja ya vipaumbele, haswa Mashariki mwa Kongo na huko Katanga.

Pamoja na masuala ya usalama, masuala ya kijamii maendeleo, elimu kwa wote. Tuligusia mengi kuhusu mageuzi kwani yanahitajika katika sekta kadhaa," alisema Kyenge. **DW**

# Buhari ampongeza Okonjo-Iweala mkuu mpya WTO

**Abuja,** NIGERIA

RAIS wa Nigeria, Muhammadu Buhari, amempongeza Ngozi Okonjo-Iweala kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO).

Katika taarifa yake, Buhari alisema kwamba rekodi iliyowekwa na Okonjo-Iweala ni uadilifu, bidii na nia ya maendeleo kwa wanadamu katika jukumu kubwa la kuhudumia dunia.

"Dk. Okonjo-Iweala, ambaye kwa miaka mingi aliweka rekodi kubwa za mageuzi ya kiuchumi nchini Nigeria.

Akiwa waziri wa fedha, baadaye waziri wa masuala ya kigeni, atastawi katika mamlaka hii na aithibitishie dunia kwa kuimarisha taasisi hii ya kimataifa, kuliko wengine," alisema Buhari.

Wanachama wa shirika hilo, juzi usiku, walimteua Okonjo-Iweala, aliyekuwa waziri wa zamani wa fedha wa Nigeria awamu mbili, kuwa mkurugenzi mkuu WTO na kumpa jukumu la kulifufua shirika lenye wanachama 164.

**WTO inaweza kuchangia sana kwa kudhibiti janga hilo. Hakuna aliye salama hadi kila mmoja awe salama.**

Okonjo-Iweala (66), atahitaji kushawishi mazungumzo ya biashara ya kimataifa wakati kukiwa na mzozo unaoendelea kati ya Marekani na China.

Pia atatakiwa kujibu shinikizo la mageuzi ya sheria za biashara na kinga ya kukabiliana na ongezeko la janga la corona.

Aidha, mkurugenzi huyo, alisema hali ya utaifa katika chanjo ya COVID-19 kwa mtazamo wake utazorotesha maendeleo katika kutokomeza janga hilo na kukwamisha ukuaji wa uchumi kwa nchi zote, ikiwamo tajiri na maskini.

Katika mahojiano na Shirika la Habari la Reuters, Okonjo-Iweala, alisema kipaumbele chake katika WTO ni kukabiliana na corona, kwamba nchi wanachama ziharakishe mchakato wa kuondoa vizuizi vya usafirishaji wa bidhaa, ambavyo vinazorotesha biashara, ugawaji dawa na vifaa.

Okonjo-Iweala ataanza kazi yake mpya Machi Mosi, mwaka huu.

"WTO inaweza kuchangia sana kwa kudhibiti janga hilo," Okonjo Iweala amesema. Hakuna aliye salama hadi kila mmoja awe salama."

Alisema utafiti unaonyesha uchumi wa dunia utapoteza Dola trillioni tisa katika mapato yanayotarajiwa, ikiwa nchi maskini zitashindwa kuchanja raia wake huku nchi tajiri zitajitwisha nusu ya athari hizo. **XINHUA/VOA**



Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala, walipokutana katika moja ya mikutano ya kimataifa. **PICHA: MAKTABA**

# 60 wafa maji boti ikizama Mto Congo

**Kinshasa,** DRC

MAOFISA wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wamesema zaidi ya watu 60 wamezama na 200 hawajulikani walipo.

Hiyo ni baada ya mashua kupinduka na kuzama katika Mto Congo na kwamba watu 300 waliokolewa.

Wakazi walisema boti iligonga mwamba Mashariki mwa mji mkuu Kinshasa, wakati walipokuwa wakisafiri usiku.

Safari za majini nyakati za usiku zilikwishapigwa marufuku nchini humo.

Waziri wa Masuala ya Kibinadamu, Steve Mbikayi, alitaka wale wamiliki wa boti hiyo kushtakiwa.

"Chombo kilichojaa kupita kiasi, kilichokuwa na abiria zaidi ya 700 kilipinduka Mai-Ndombe. Miili 60 tayari imepatikana na watu 300 walinusurika, tunazipa pole familia zilizofiwa na tunataka hatua zichukuliwe dhidi ya wale wote wanaohusika na sekta ya uchukuzi," aliandika waziri huyo kwenye mtandao wa Twitter.

Barabara ni chache DRC na shughuli nyingi za usafirishaji wa mizigo na abiria hufanywa kwa njia ya mto au ziwa. **BBC**



# NEWCASTLE YAPEWA OFA KUMSAJILI STURRIDGE

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle imepewa ofa ya kumsajili huru straika, Daniel Sturridge kwa kipindi cha msimu kilichobaki.

Sturridge amekuwa hana timu tangu Machi 2020, wakati mkataba wake na klabu ya nchini Uturuki ya Trabzonspor ulipotenguliwa ikiwa ni miezi sita tu tangu awe na timu hiyo.

Sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, Sturridge amekuwa akijifua kwa ajili ya kurudi dimbani, huku pia akitajwa kuwaniwa na klabu za Ligi Kuu Marekani, MLS.

Lakini kwa mujibu wa 90min, Sturridge mwenyewe bado anaamini kwamba ana nafasi nzuri zaidi ya kurudi kucheza kwenye Ligi Kuu England.

West Bromwich Albion na Sheffield United zote zimewasiliana na Sturridge, lakini sasa Newcastle ambayo imempoteza straika wake nyota, Callum Wilson kwa majeruhi wamepewa nafasi ya kumsajili nyota huyo wa zamani wa Liverpool.

Wilson anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi miwili, akiwaachia Steve Bruce na Joelinton, Andy Carroll na Dwight Gayle kama ndio mastraika waliobaki.



# Mo Salah: Liverpool bado ina nafasi EPL

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah anaamini kwamba, Liverpool bado ina nafasi ya kutetea taji la Ligi Kuu England msimu huu.

Nyota huyo wa kimataifa wa Misri anaona kwamba timu yake hiyo ina nafasi ya kufanya vizuri na kuweza kutwaa taji hilo tena kwa msimu huu licha ya kuwa kwenye mwendo wa kusuasua hivi karibuni.

Salah ndio kinara wa utupiaji akiwa ametupia jumla ya mabao 17 msimu wa 2020/21, timu yake ya Liverpool ipo nafasi ya nne.

Timu hiyo kwa sasa inapambana kutetea taji la Ligi Kuu England ililotwaa msimu uliopita wa 2019/20 chini ya Jurgen Klopp.

Anafuatiwa kwa ukaribu na nyota wa Manchester United, Bruno Fernandes ambaye amefunga jumla ya mabao 14 na timu yake ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi 46.

Kinara wao ni Manchester City ya Pep Guardiola ikiwa na pointi 53 baada ya kucheza jumla ya mechi 23.

Salah amesema: "Wengi wapo nyuma yetu wanapenda kuona tunafanya vizuri hilo lipo wazi na tunaamini kwamba tunaweza kufikia malengo hayo na tutafanya vizuri katika kutetea taji.

"Kwa sasa hatupati matokeo mazuri, lakini naamini tuna nafasi ya kuweza kutetea taji la Ligi Kuu England."

# Arsenal kumpa tena mkataba mpya Luiz

**LONDON,** England

MLINZI wa kati wa Arsenal, David Luiz anatarajiwa kuongezewa mkataba mpya wa kuendelea kubaki hapo kwenye dimba la Emirates.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ameingia kwenye miezi yake sita ya mwisho ya mkataba wake wa sasa na majaliwa yake yalikuwa hayajulikani kwa 'Washikabunduki' hao wa London.

Luiz amekuwa hana uhakika wa namba kwenye kikosi cha Arsenal msimu huu, kwani kuna wakati kiwango chake kimekuwa si cha kuvutia.

Na sasa kocha, Mikel Arteta ameonekana kuvutiwa na kiwango cha Luiz na kushawishi aongezewe mkataba.

Baada ya kutumikia adhabu ya kuoneshwa kadi nyekundu kwenye mchezo wa kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Wolves, Luiz alionyesha kiwango cha kuvutia kwenye mchezo wa ushindi wa 4-2 wa Jumapili dhidi ya Leeds.

Arteta anaona kwamba, Luiz anaweza kuwa patina mzuri wa Rob Holding kwenye safu ya ulinzi.



# Klopp akataa kujiuzulu Liverpool

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesisitiza yeye na wachezaji wa Liverpool wapo tayari kupambana na kubadilisha matokeo, huku akikataa kabisa kwamba anaweza kuwa tayari kuondoka pale Anfield.

Kichapo cha mabao 3-1 mwishoni mwa wiki kutoka kwa Leicester City, baada ya Mohamed Salah kuwapa bao la uongozi 'Wekundu' hao pale kwenye dimba la King Power, Klopp alikiri kwamba mabingwa hao watetezi hawawezi kupambana na vinara Manchester City kwenye mbio za ubingwa.

Katika mechi ya awali, Liverpool walichezea kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa City, ambapo waliwazidi pointi 13 huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi.

Uvumi ulienea kwamba, baada ya kipigo hicho cha Leicester, Klopp angeachia ngazi ndani ya kikosi hicho.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 53 mama yake mzazi, Elisabeth alifariki wiki iliyopita lakini alishindwa kwenda kumzika kutokana na sheria sa usafiri kwa kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona.

Licha ya kukutana na bango nje ya uwanja lililokuwa linamtaka Klopp kuachia ngazi, lakini yeye ameweka wazi kwamba, wataendelea kupambana.

"Bango ni zuri, si muhimu nafikiri. Sihisi kama nahitaji sapoti maalumu kwa wakati, lakini ni wakati mzuri kujipanga," alisema Klopp kuelekea mchezo wa jana wa Ligi ya Mabingwa Ulaya utakaopigwa mjini Budapest.

"Nini kilikuwa kitu kingine? Kwamba naweza kufukuzwa au kuondoka au nini zaidi? Sihitaji mapumziko kwa sasa."






# BAO LA WERNER LAMKUNA TUCHEL

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel anaamini bao la Timo Werner dhidi ya Newcastle United litampa straika huyo wa Chelsea "asilimia ya kuaminiwa."

Werner alimaliza kusubiri kufunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu England tangu Novemba 7, mwaka jana, waliposhinda dhidi ya Sheffield United, kwa kuifungia bao la pili Chelsea wakati wakiibuka na ushindi wa 2-0.

Nyota huyo wa zamani wa RB Leipzig alitengeneza bao la kwanza lililofungwa na Olivier Giroud na yeye akaongeza la pili akifunga kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha dakika 1,000.

"Kwa washambuliaji, asilimia ya kuaminiwa inakuja kutokana na mabao," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Anajituma sana, na alipambana haswa. Leo (juzi) ametoa pasi ya mwisho na kufunga bao, ni kitu kizuri, kizuri sana kwake."

Tuchel, anaamini Chelsea hawakuwa vizuri sana ndani ya boksi na kutaka kuimarika zaidi kuelekea mechi dhidi ya Atletico Madrid na Manchester United.

Aliiambia Sky Sports: "Nilikipenda kipindi cha kwanza, ambapo tulicheza kwa bidii kubwa na kujituma na tuligusa mipira mingi kwenye boksi na kupiga mashuti.

# Costa akaribia kutua Palmeiras

**LIVERPOOL,** England

STRAIKA wa zamani wa Atletico Madrid, Diego Costa, yupo kwenye mazungumzo na klabu ya nchini Brazil ya Palmeiras baada ya kuondoka pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano.

Costa amecheza mechi saba tu kwa Atletico katika nusu ya kwanza ya msimu huu, akifunga mabao mawili, kabla ya kusitisha mkataba wake Desemba mwaka jana.

Mpango wa kurudi kwenye Ligi Kuu England ulishindika Januari, na sasa Sky Sports News imebainisha kwamba, Costa yupo kwenye mazungumzo na Palmeiras, klabu ambayo alikuwa akiishabikia wakati akiwa mtoto alipokuwa akiishi Brazil.

Klabu hiyo imeripotiwa kumpa ofa ya mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya pauni milioni 2.6 kwa msimu.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca la nchini Argentina, dili hilo linaweza kukamilika mapema wiki hiii.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Globo Esporte, Palmeiras bado wanajaribu kutaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kupunguza kiasi cha mshahara anachokitaka.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAMTENGEA DAU NONO HAALAND

**Euro milioni 90 zatengwa huku Luka Jovic ama Mariano Diaz wakitarajiwa kugeuzwa chambo...**

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imeripotiwa inapanga kutoa kiasi cha euro milioni 90 kwa ajili ya kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland kuelekea msimu ujao.

**Haaland mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akiwaniwa na klabu kubwa barani Ulaya baada ya kung'ara kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.**

Na sasa Madrid ipo tayari kuhakikisha inamsajili Haaland kuelekea msimu mpya wa 2021-22.

Kwa mujibu wa ABC, Real Madrid tayari imeshawasilisha ofa mezani kwa Borussia Dortmund ya euro milioni 90, ili kuhakikisha inamtwaa Haaland.

Ripoti za nchini Hispania zinaeleza kwamba, miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, watajaribu kumchukua Luka Jovic, ambaye anacheza kwa mkopo kule Eintracht Frankfurt, au Mariano Diaz kuwa sehemu ya dili hilo.

Haaland amefunga mabao 23 kwa Dortmund msimu huu pekee, na anaonekana kuwa lulu kubwa barani Ulaya kwa wachezaji vijana.

Klabu za Manchester United, Manchester City na Chelsea ni miongoni mwa timu ambazo nazo zimekuwa zikitajwa kuwania saini ya nyota huyo.

Kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer ambaye ni raia mwenzake wa Norway msimu uliopita alijaribu kumshawishi Haaland kujiunga na klabu hiyo, lakini aligonga mwamba.

Lakini inaaminika kwamba, bado anaendelea kumfuatilia kwa ajili ya kumshawishi kujiunga na 'Mashetani Wekundu' hao.

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL, SPURS KWA KONSA

LIVERPOOL na Tottenham Hotspur zinamfuatilia kwa karibu mlinzi wa Aston Villa, Ezri Konsa, 23, zikiwania kumsajili kipindi cha majira ya joto, mchezaji huyo wa England chini ya umri wa miaka 21. ***(Athletic)***

### HOPPE AVUTIA NYINGI EPL

LIVERPOOL, Manchester United, Manchester City na Tottenham Hotspur zinamfuatia straika wa Schalke raia wa Marekani, Matthew Hoppe, 19. ***(90min)***

### MBAPPE AWAPASHA PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, ameiambia Paris St-Germain anataka kumaliza mkataba wake, ambao unafikia mwisho kipindi cha majira ya joto 2022. ***(Sport - in Spanish)***

### MOURINHO NA KIBARUA CHAKE

NAFASI ya kocha wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho haipo shakani, lakini matokeo ya timu hiyo yanaonekana kutowafurahisha mabosi wake. ***(Mail)***

### GUNDOGAN AFIKIRIA UKOCHA

KIUNGO wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan, 30, amesema anataka kuingia kwenye uongozi wa soka mara atakapomaliza kipindi chake cha uchezaji. ***(Goal)***

### LINGARD SIKUPEWA NAFASI UTD

KIUNGO wa West Ham na England, Jesse Lingard, 28, amesema "hakupata nafasi" pale Manchester United wakati soka liliposimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. Mchezaji huyo anacheza kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu. ***(BT Sport)***

### FA KURUDISHA MASHABIKI

FAINALI za Kombe la FA na Carabao zinatumika kama jaribio la kuwarudisha mashabiki uwanjani nchini England. ***(Times)***

### COOPER ATAJWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace imemtaja kocha wa Swansea, Steve Cooper kama ndiye anaweza kuwa mrithi wa Roy Hodgson. ***(Sun)***

### ALABA APEWA OFA CHELSEA

CHELSEA ndio klabu pekee iliyotoa ofa ya mkataba kwa mlinzi wa Bayern Munich na Austria, David Alaba, 28, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(90min)***

### FULGINI AWANIWA SOUTHAPTON

KLABU ya Southampton inawania kumsajili kiungo wa Angers, Angelo Fulgini, 24. Awali walijaribu kumsajili Januari mchezaji huyo. ***(Le10 Sport)***

### BEI YA AARONS YATAJWA

NORWICH imeitaarifu Bayern Munich kwamba, watakiwa kulipa pauni milioni 30 hadi 35 kama wanataka kumsajili Max Aarons, 21. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

# MBRAZIL ASIFU VIWANGO VYA MAKIPA SIMBA KUIMARIKA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa makipa wa klabu ya Simba, Milton Nienov, amesema viwango vya makipa wote watatu wa Simba kwa sasa viko juu, tofauti na mwanzo alivyokuja.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, kocha huyo Mbrazil ambaye alijiunga na Simba mwanzoni mwa mwaka huu, alisema makipa wote aliuowakuta kwenye kikosi hicho ni wazuri, lakini alichofanya ni kuwaongezea mbinu ambazo zitawafanya waonekane bora.**

Simba ina makipa watatu ambao ni Aishi Manula, Beno Kalolanya na Ally Salim.

"Hakijaongezeka kwa Manula tu, au kwa Kakolanya, ila hata kwa Ally, naye ameongezeka kiwango na kama akipata nafasi ataonyesha kile ambacho amekipata," alisema kocha huyo.

Mashabiki wengi wa soka nchini kwa sasa wameonekana kukoshwa na kiwango cha hali ya juu cha Manula akiwa na Simba pamoja na timu ya Taifa, Taifa Stars.

Manula ambaye kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika amecheza mechi nne bila wavu wake kutikiswa, lakini alitia fora kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN) zilizomalizika hivi karibuni nchini Cameroon.

Kwa miaka ya hivi karibuni, Manula alikuwa akituhumiwa kushuka kiwango kwa kuruhusu mabao rahisi akiwa kwenye timu ya taifa na hata akiwa na Simba.

Na hii ilisababisha hata viongozi wa Simba, pamoja na mambo mengine, kubadilisha kocha wa makipa ambaye wakati huo alikuwa Mwarami Mohamed, kabla ya kumtwaa Mbrazil huyo.

Manula hakufungwa kwenye mechi za awali kati ya Simba dhidi ya Plateau United, timu yake ikishinda bao 1-0 ugenini na suluhu nyumbani, ikishinda mabao 4-0 nchini Tanzania dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe, na ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya AS Vita ya DR Congo.

NAWATOKA...




Mshambuliaji wa KMC, Charles Ilanfya, akiwatoka wachezaji wa timu ya Mwadui FC katika mchezo wa Ligi Kuu uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Namungo yaeleza hatima ya Kikoti, wenzake*

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU ikimshukuru Mungu baada ya kurejea nchini salama, uongozi wa Klabu ya Namungo umeeleza hatima ya wachezaji wake watatu na kiongozi mmoja waliyowekwa karantini nchini Angola, baada ya kudaiwa kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Ijumaa iliyopita Kikosi cha Namungo FC kilipata misukosuko kwa kuzuiliwa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Luanda, Angola huku wachezaji wote na viongozi wakitakiwa kukaa karantini kwa muda wa siku tatu, baada ya mamlaka nchini humo kudai wachezaji watatu na kiongozi mmoja wana maambukizi ya virusi vya corona walipotua huko kwa ajili ya mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Clube Desportivo 1º de Agosto, kuwania kufuzu hatua ya makundi.

Hata hivyo, mechi hiyo haikuchezwa kutokana na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), kuifuta hadi hapo kamati yake itakapotoa uamuzi kutokana wenyeji kukiuka kanuni kadhaa za mashindano hayo.

Wachezaji waliodaiwa kukutwa na maambukizo ya virusi vya corona na ambao hadi sasa wapo karantini nchini Angola ni Lucas Kikoti, Fred Tangalu na Khamis Faki pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo (CEO), Omary Kaaya.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Hassan Zidadu, alisema wachezaji wote wapo salama na kutoa shukrani kwa Watanzania kutokana na ushirikiano waliowaonyesha tangu mwanzo wa matatizo mpaka sasa.

"Tumefika jana [juzi] saa tatu usiku tupo salama wachezaji tuliokuja nao wapo vizuri tunachokisubiri kwa sasa ni uamuzi kutoka CAF, tunawaomba Watanzania wazidi kuwa wavumilivu," alisema Zidadu.

Kuhusu wachezaji waliowaacha Angola, alisema wanawasiliana nao na wanaendelea vizuri na kwamba Serikali ya Angola imewaahidi kuwapa ulinzi wa kutosha ikiwamo kuwalipia gharama zote za usafiri wa kuwarudisha nyumbani.

"Angola wametuhakikishia kuwapa uangalizi mzuri wachezaji wetu tuliowaacha pamoja na kutuhakikishia watarudi salama nyumbani," alisema.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema kikosi cha Namungo kitaendelea kubaki jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na majukumu mengine.

## Mtibwa yamhofia Katwila ikiivaa Ihefu FC

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Mtibwa Sugar, Baraka Majogoro atakosa mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu FC itakayopigwa leo katika Uwanjani wa Jamhuri mjini Morogoro, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thierry Hitimana, alisema Majogoro atakosekana katika mchezo huo kwa sababu ya kukabiliwa na matatizo ya kifamilia kwa kufiwa na mdogo wake.

Alisema wachezaji wengine wako fiti na tayari kwa ajili ya mchezo huo ambao wamepania kubakiza pointi tatu wakiwa uwanja wao wa nyumbani.

"Mechi dhidi ya Ihefu FC ni ngumu kwa sababu kocha na mpinzani wetu, Zuberi Katwila aliwahi kuifundisha Mtibwa Sugar hivyo anawafahamu wachezaji wetu, lakini nao wanafahamu mbinu za kocha huyo.

"Lazima tupambane tushinde nyumbani, tusipopata matokeo mazuri katika mechi hiyo, itakuwa ngumu kupata matokeo ugenini, nawaheshimu Ihefu FC kwa sababu nao wamepata matokeo mazuri ugenini kwenye mechi iliyopita dhidi ya Ruvu Shooting, hivyo wana morali ya juu," alisema Hitimana.

## JKU, KVZ zaanza vema Kombe FA

**Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU za Ligi Kuu Zanzibar, JKU na KVZ zimesonga mbele katika michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup baada ya juzi kuibuka na ushindi kwenye michuano hiyo iliyoanza kutimua vumbi juzi.

JKU iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Super Tiger katika Uwanja wa Wimbi, huku timu ya KVZ ikiifunga Jang'ombe Boys mabao 2-0 mchezo uliochezwa katika Dimba la Amaan.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa timu ya JKU, Omar Khamis "Matu" alisema lengo lake ni kuhakikisha kufanya vizuri zaidi katika mashindano hayo.

Alisema anajua michuano hiyo kadri inavyosonga mbele itakuwa migumu kutokana na kukutana na timu za madaraja ya chini kwa sasa(mikoa na daraja la kwanza Kanda).

Aidha, alisema timu yake inaendelea kujinoa kuelekea michezo ya Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa pili na mashindano hayo ya Kombe la FA CUP katika michezo inayofuata.

# Michezo

Jumatano Februari 17, 2021

Nipashe




Madrid yamtengea dau nono Haaland UKURASA 22

# Fiston kufuta makosa Yanga kwa Kagera?

## ●●● Ni mechi ngumu ya nguvu na ufundi, Kaze na Maxime wasema...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kushindwa kuonyesha cheche zake kwa kuisaidia timu yake ya Yanga kuibuka na ushindi akiichezea kwa mara ya kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbeya City Jumamosi iliyopita, leo mshambuliaji mpya wa kikosi hicho, Fiston Abdoulrazak, atakuwa na nafasi nyingine ya kufuta makosa yake wakati timu hiyo itakapoikaribisha Kagera Sugar katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Katika mechi iliyopita ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 ikichezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Fiston alianza kikosi cha kwanza, lakini hakuweza kucheka na nyavu wala kuwa na madhara makubwa katika safu ya ulinzi ya Mbeya City.**

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema bado ni mapema kuanza kumtupia lawama mshambuliaji huyo aliyejiunga na timu hiyo katika usajili wa dirisha dogo Januari mwaka huu.

Kaze alisema uwanja kutokuwa rafiki kwa ujumla kulichangia timu yake kushindwa kuonyesha soka safi, lakini leo kikosi hicho kitakuwa katika uwanja bora kabisa nchini na Afrika Mashariki wa Mkapa, hivyo itakuwa nafasi nzuri kwa Fiston kuonyesha ubora wake na kuisaidia timu hiyo kupata matokeo, endapo atapewa tena nafasi ya kuanza.

Akizungumza na mwandishi wetu Fiston alisema anaamini kwa ubora wa wachezaji wanaounda kikosi cha Yanga akishirikiana nao vema wanaweza kupata matokeo chanya kwa kufunga mabao wanapopata nafasi.

"Kwa ujumla ushindani ni mkubwa na kila timu inahitaji kupata matokeo chanya ndani ya uwanja, bado tuna muda wa kufanya vizuri na mashabiki watafurahi," alisema.

Yanga na Kagera Sugar zitashuka dimbani leo zote zikitoka kulazimishwa sare katika mechi zilizopita ambapo 'Wakata Miwa' hao wa Kagera walilazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani na Gwambina FC.

Akizungumzia mechi hiyo, Kaze alisema kawaida mzunguko wa pili huwa ni mgumu zaidi, hivyo haitakuwa mechi rahisi kwa kila upande licha ya kwamba wamejipanga kupata matokeo chanya ili kutimiza malengo yao ya kutwaa ubingwa msimu huu.

"Tumefanyia kazi kasoro zilizojitokeza mechi iliyopita na tunaamini tunaweza kufanya vizuri kesho (leo)jioni (jana) tutaendelea na maandalizi ya mwisho kwani tunahitaji kupambana kuhakikisha tunafikia malengo yetu," alisema Kaze.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema kikosi chake kipo tayari kwa mchezo huo na kila mchezaji anafahamu wanachokitafuta ni ushindi tu.

"Kila timu inapocheza inachotaka ni ushindi, hayo ndiyo malengo yetu pia katika mechi hiyo, tutapambana na tunaamini tutaonyesha mchezo bora," Maxime.

Yanga itashuka dimbani ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo na pointi 45 baada ya kucheza mechi 19 sawa na Kagera Sugar yenye alama 23 katika nafasi ya 10.



Fiston mazoezini. **MPIGAPICHA WETU**

# TFF, Azam kufunga taa viwanja vinne Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF) kwa kushirikiana na mmoja wa wadhamini wa Ligi Kuu, Azam Media, wanatarajia kufunga taa kwenye viwanja vinne Tanzania ili kuwezesha mechi kuchezwa usiku na kuepuka michezo ya saa nane mchana kutokana na ufinyu wa ratiba.

Kwenye Mkutano wa TFF, Azam Media na waandishi wa habari uliofanyika jana, viwanja ambavyo vitapata bahati ya kuwekewa taa ni Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi, Uwanja wa Gwambina uliopo Misungwi mkoani Mwanza, Uwanja wa Kaitaba uliopo Bukoba mkoani Kagera na Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Akizungumza kwenye mkutano huo jana, Injinia Victor Ndozelo kutoka Azam, alisema kuwa tayari mradi huo mkubwa umeshaanza kufanya kazi kwa kuanza kukagua viwanja hivyo na kujiridhisha kuwa kazi hiyo itafanyika kwa ufanisi mkubwa.

"Tangu Agosti mwaka jana tulianza kutembelea viwanja ambavyo tuliona vina sifa ya kuwekewa taa.

Kwanza tuliangalia viwanja ambavyo vina sehemu nzuri ya kuchezea 'pitch', halafu pia tukaangalia tuwekeze kwenye timu ambazo zinajituma kwenye ligi na zina uhakika wa kubaki Ligi Kuu.

Hivyo ndivyo vigezo kwa kuanza tulivyotumia, lakini tulikuwa tukikagua udongo kwa ajili ya kupata vipimo, kwani tutaweka nguzo za taa na si kila udongo unaweza kubeba nguzo hizo," alisema Injinia huyo.

9 770856 541002 >